**Serikali** yatangaza ajira mpya 44,000, upandishaji

UKURASA 5




**Madereva** Dangote sasa warejea kazini, maslahi kuboreshwa

UKURASA 19


# Nipashe

Ijumaa Aprili 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580559

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Alaba mambo safi Real Madrid**

UKURASA 21

# MWENDO ULEULE

• **Rais** Samia ahutubia Bunge dakika 92, asisitiza anaweza, anajiamini...*Uk.2,3 na 4*

## MAMBO MUHIMU

- **Mishahara juu, madaraja kupanda**
- **Kukutana na vyama vya siasa**
- **Bunge ruksa kuikosoa serikali**
- **Kukuza usawa kijinsia, uteuzi wanawake zaidi**
- **ATCL kulelewa kimkakati, kulitua mzigo wa deni**
- **Wahandisi maji mikoani kufumuliwa**
- **Ushirikiano kimataifa kuboreshwa**
- **Vitambulisho machinga kuja kivingine**
- **Wezi, wabadhirifu kushughulikiwa**
- **Mashirika ya umma kujiendesha kwa tija**
- **Corona; kila mtu ajilinde**
- **Wanaotumia mitandao ya kijamii vibaya kusakwa**
- **Sekta muhimu kiuchumi kupewa kipaumbele**



Rais, Samia Suluhu Hassan, akilihutubia Bunge jijini Dodoma jana. **Picha chini;** wananchi wakifuatilia hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan, eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: BUNGE/JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **RAIS SAMIA AAHIDI KUPAISHA MICHEZO** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6





Rais Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride maalum la Jeshi la Polisi, lililoandaliwa kwa ajili yake, kabla ya kulihutubia Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Demokrasia kuimarishwa

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu amesema amepanga kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja kuimarisha demokrasia na ustawi wa siasa nchini.

Katika hotuba yake ya jana bungeni, Rais Samia alisema ameona kuna haja kukutana na viongozi hao ili kuzungumza nao namna ya kwenda kidemokrasia.

"Ninakusudia kukutana na viongozi wa kisiasa wa Tanzania, ili kwa pamoja tuweke msimamo wa kuendesha shughuli za kisiasa," Rais Samia alisema.

**HABARI, CORONA**

Kuhusu uhuru wa habari, Rais Samia alisema: "Hakuna uhuru usio na haki. Tunahitaji uhuru wa vyombo vya habari na kuongeza ujuzi wa kidiplomasia kimataifa.

"Katika eneo la kidiplomasia, tutawatumia watu wenye weledi na ujuzi katika eneo hili."

Rais Samia pia alizungumzia ugonjwa wa corona akiwakumbusha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa ugonjwa huo bado haujapatiwa tiba.

Alisema wataalamu wa ndani wanaendelea kushirikiana na wataalamu wengine wa nje wanaotoka katika jumuiya za kikanda na kimataifa kuweka mikakati ya pamoja kukabiliana na virusi hivyo.

# Samia asisitiza mwendo ni ule ule

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaonya wala rushwa, mafisadi, warasimu, wazembe na kuwaeleza kwamba ataendeleza mwendo ule ule aliouacha Hayati Rais John Magufuli.

Amesema Hayati Rais Magufuli ameondoka peke yake na kuacha maono, falsafa, mikakati, ambayo bado inafanya kazi na kuonya kuwa wanaodhani kwamba ameondoka na vitu hivyo wanajidanganya.

Samia alitoa onyo hilo jana jijini Dodoma wakati akilihutubia Bunge na kueleza kuwa Tanzania ilipofika sasa haitakubali kurudi nyuma.

Katika hotuba hiyo ya saa moja na dakika 32, alisema: "Kuna baadhi ya watu wameanza kugeuka wakiwamo wawekezaji, niwape taarifa kwamba mwendo ni ule ule aliouacha Hayati Rais Magufuli," alisema.

Kadhalika, Rais Samia aliwaonya watumiaji wa mitandao ya kijamii kuacha tabia ya kuweka taarifa za upotoshaji juu ya kifo cha Hayati Rais John Magufuli, kwamba kuna watu wamemuua.

Akitoa ufafanuzi wa kifo cha Hayati Rais Magufuli, Rais Samia alisema madaktari waliokuwa wanamtibu Hayati Rais Magufuli wameeleza kwamba alifariki dunia kwa tatizo la udhaifu wa moyo, ambalo ameishi nalo kwa zaidi ya miaka 10.

"Naona katika mitandao ya kijamii watu wanasema fulani, fulani wamempa sumu. kama wana taarifa za maana waje tuwasikilize. Tuna vyombo vya ulinzi, waje tuwasikilize, vinginevyo wanyamaze.

"Waache kuleta uchonganishi katika nchi, kama wanadhani hatutawapata basi warudi kwa Mungu na wajiulize kama wanavyofanya ni kweli?," alisema Rais Samia.

**ASISITIZA ANAWEZA**

Kadhalika, Rais Samia aliwajibu watu wanaosema kwamba hataweza kutimiza yale anayoyasema kwenye hotuba yake kwa sababu yeye ni mwanamke.

"Naomba niwaambie kwamba Mungu hakuumba ubongo hafifu kwa mwanamke na ubongo makini kwa mwanamume. Jamii iliyokuzunguka pamoja na makuzi ndivyo vinavyokubeba na kukujenga. Nimekuzwa kwenye jamii makini na nina uzoefu wa kutosha serikalini na ndani ya chama. Ninajiamini ninaweza kuliongoza taifa hili," alisema Samia.

Rais Samia alisema yote aliyoyasema hatatekeleza peke yake bali kwa kushirikiana na Watanzania. Hivyo, aliwataka Watanzania kuwa na upendo, mshikamano katika kufanikisha kuyatimiza yote anayoyasema.

**MISHAHARA, VYEO**

Samia pia alikata kiu iliyodumu kwa muda mrefu juu ya watumishi wa umma kutopandishiwa mishahara na madaraja huku akiahidi kwamba vitafanyiwa kazi katika uongozi wake.

Alisema kilio cha watumishi wa umma katika mambo hayo kimekuwa cha muda mrefu na kwamba serikali yake imekisikia.

# ...alivyoingia bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NDEREMO na vifijo vilitawala bungeni wakati Rais Samia akiingia ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria, msafara wake ukiongozwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai,

Wakati kiongozi huyo anaingia kwenye Ukumbi wa Bunge, baadhi ya wabunge walikuwa wanaimba 'tuna imani na Samia; huku wimbo wao huo ukichagizwa na kugonga meza, ikiwa ni ishara ya kukubaliana na jambo fulani.

Rais Samia aliingia ukumbini saa 9:55 alasiri baada ya kukagua gwaride maalum lililoandaliwa kwa ajili yake kwenye Viwanja vya Bunge.

**ULINZI WAIMARISHWA**

Ulinzi ulikuwa umeimarishwa katika Viwanja vya Bunge, viongozi wote wakipitia Geti A la Bunge ambalo linatazamana na Barabara ya Morogoro.

Kutokana na viongozi kutumia geti hilo, barabara hiyo ilifungwa kwa muda kuruhusu viongozi kuingia bila mwingiliano wa magari mengine.

**SUTI ZATAWALA**

Watumishi na maofisa wa Bunge walikuwa wamevaa mavazi nadhifu huku vazi la suti za rangi ya nyeusi na bluu na iliyokoza yakitawala.


Kabla Rais hajaingia ukumbini, wabunge waliingia ukumbini saa nane mchana kutokana na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuwataka wawe wamekaa kwenye ukumbi saa 9:00 alasiri.

Viongozi waliohudhuria bungeni jana ni pamoja na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah. Wengine ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof.Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Martin Ngoga, na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ally Maulid.

Viongozi wastaafu waliokuwapo ni pamoja na marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Jakaya Kikwete, Amani Abeid Karume, Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wastaafu, Mohamed Gharib Bilal, mawaziri wakuu wastaafu John Malecela na Fredrick Sumaye, maspika wa Bunge na Baraza la Wawakilishi wastaafu, wake za marais wastaafu, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na wakuu wa taasisi za umma.







Wabunge wakiwa wamesimama wakati Rais, Samia Suluhu Hassan akiingia bungeni, jijini Dodoma jana, akiongozwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rais Samia awaibua viongozi wa dini, wabunge wafanyabiashara

**Na Waandishi Wetu**

HOTUBA ya Rais Samia aliyoitoa Bungeni jana, imepokewa kwa mtazamo chanya na kupongezwa na watu mbalimbali wakiwamo maaskofu, wabunge na wafanyabiashara.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema uamuzi wa Rais Samia kutaka kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini, una nia njema ya kutibu majeraha ya kisiasa.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, baada ya Rais Samia kumaliza kulihutubia Bunge, Dk. Shoo alisema: "Nimeona mama (Rais Samia) ametoa hotuba nzuri sana. Inaonyesha mwelekeo mzuri kwa taifa na inawatia watu matumaini. Mimi nampongeza kwa hotuba nzuri.

"Kwangu kubwa ni hilo la kusema atakutana na viongozi wa vyama vya siasa ni jambo jema sana na mimi ninampongeza kwa hilo. Nina amini ni sehemu ya kuonyesha majeraha aliyoyasema katika hotuba yake alipokuwa akiapishwa kuwa Rais wa sita."

Kuhusu suala la utendaji haki kwa mahakama, Dk. Shoo alieleza: "Hilo ni jambo ambalo limekera Watanzania wengi. Kwa mahakama kutenda ule wajibu wake wa kusimamia haki na kuona kwamba haki inatendeka."

"Kwa hilo la uzushi kwenye mitandao ya kijamii hata sisi tunasema linatukera sana. Mahali pengine tumejaribu hata kukemea pale ambapo watu wanatumia mitandao ya kijamii kupeleka taarifa ambazo hazina ukweli ndani yake.

Na pale ambapo zinatumika kwa malengo ya kuchonganisha. Lazima tuwe na maadili na kuwe na matumizi ya taarifa tunazoweka katika mitandao pamoja na kwamba ni kitu kizuri cha kupashana habari," alisema.

**ASKOFU BAGONZA**

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alipotakiwa kutoa maoni yake kuhusu hotuba ya Rais Samia, alisema ni jambo zuri kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini, lakini akiwa kiongozi wa dini, anamuunga mkono na anampongeza kwa uamuzi huo.

"Ni jambo zuri kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini, kwa hiyo ni namna gani anaweza kuzungumza na viongozi wa vyama vya siasa, tunasubiri kuona jinsi gani atakavyofanya.

"Tusubiri tuone anaongea nini, kwa sababu kukutana ni jambo moja na nizuri lakini anaongea nini nao, hilo ni jambo jingine."

**WABUNGE WAPONGEZA**

Mbunge wa Gairo (CCM), Ahmed Shabiby, alisema hotuba imetoa majibu ya maswali mengi na kutoa mwelekeo wa serikali atakayoiongoza ikiwamo kupandisha mishahara ya wafanyakazi, kufanya mabadiliko kwa wahandisi wa maji.

"Sekta binafsi pia iendane na sheria na vitu vingi virekebishwe kwa kuwa wanategemeana, na wawe marafiki haya maono yote hakuna litakaloshindikana," alisema.

Mbunge wa Manonga (CCM), Seif Gulamali, alisema taifa likuwa na shauku ya kusikiliza mwelekeo wake na amekata kiu ya Watanzania ikiwamo kumaliza miradi yote iliyoanzishwa na mtangulizi wake, kuboresha biashara na kufungua milango ya kuzungumza na vyama vya siasa.

Naye January Makamba (Bumbuli- CCM), alisema hotuba ya Rais inatoa mwelekeo mpya na matumaini mapya.

"Hotuba hii ni daraja kwa yaliyofanyika na yatakayofanyika, kuna muunganiko mzuri sana wa ndoto za Rais Magufuli na matumaini mapya tumefurahi kwamba mambo mazuri na mema yataendelezwa kwa msisitizo wa nidhamu na usimamizi wa mali utaendelezwa,"alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest, alisema ameanza vizuri na kuwapa moyo wanawake kwa kuongelea vitu vinavyogusa wanawake huku Halima Mdee (Viti Maalum - CHADEMA), akisema hotuba ya Rais imeonyesha mwelekeo wake na kugusa maeneo ambayo yalikuwa yamewekwa pembeni kama suala la sekta binafsi.

**WAFANYABIASHARA WALONGA**

BAADHI ya wafanyabiashara wamezungumzia hotuba ya Rais Samia kwamba ni ya matumaini makubwa hasa kwenye sekta hiyo kwa kuwa imegusa fursa zote zitakazomwezesha mwekezaji na mfanyabiashara kupanua soko la ndani na nje ya nchi.

Wamesema ni ukweli usiopingika kwamba kukosekana kwa fursa za biashara katika soko la ndani na nje ya nchi liliwanyima wafanyabiashara wa ngazi zote wakubwa na wadogo kushindwa kutanua soko la bidhaa zao.

"Kwa kweli hotuba hii imetupa matumaini makubwa sisi wafanyabiashara kuona kwamba sasa yako mazingira rafiki kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuwa na uwekezaji endelevu. Kwa muda mrefu wanfanyabiashara walishindwa kutokana na kukosa soko la uhakika wa ndani na nje ya nchi", alisema Amit Asher mmoja wa wafanyabiashara wakubwa na mwekezaji wa jijini Tanga.

Asher alisema ni wakati mwafaka sasa kwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato na utoaji wa vibali vya uwekezaji na biashara kuendana na kasi ya Rais Samia kwa kuondoa kero zinazowakabili wafanyabiashara na kupunguza urasimu kwenye sekta hiyo. Naye Raju Vasant alisema ni biashara ya mpakani kwa muda sasa zilisimama jambo ambalo liliwafanya wafanyabiashara kushindwa kufanya biashara kwenye ushindani wa soko la kimataifa.

"Tunaamini sasa sekta ya uwekezaji na biashara imepata suluhu hasa mengi aliyozungumza Rais ndiyo uhalisia wa kero zilizokuwa zikiwakabili wafanyabiashara. Tunaomba sasa utekelezaji ili tuboreshe mazingira mazuri kwa pande zote kwa maana serikali kukusanya kodi kwa ukamilifu lakini wafanyabiashara nao wafanye shughuli zao bila bugdha," alisema.

**•Imeandikwa na Na Godfrey Mushi (ARUSHA), Augusta Njoji (DODOMA) na Lulu George,TANGA**

# Wahandisi maji sasa kikaangoni

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema anakusudia kufanya mabadiliko makubwa ya uongozi katika Sekta ya Maji, akiweka wazi kuwa wahandisi wa maji mikoa watahusika kwa kiasi kikubwa.

Amesema uamuzi huo utafanyika baada ya kubaini kutokuwapo kwa ufanisi katika miradi ya maji inayotekelezwa na serikali kwa mabilioni ya shilingi.

Rais alisema anakwenda kufanya mabadiliko makubwa ya wahandisi wa maji kwenye mikoa kwa sababu tatizo bado ni kubwa na linachangiwa na usimamizi usioridhisha wa miradi na ubadhirifu wa fedha.

Alisema miradi mingi imekuwa ikitekelezwa kwa kutumia fedha nyingi lakini ndani ya muda mfupi maji hayapatikani.

"Katika miaka hii mitano tunaweka mkazo mkubwa wa kuimarisha usimamizi kwenye utekelezaji wa miradi ya maji, hapa niseme ninakwenda kufanya mabadiliko makubwa ya wahandisi wa maji huko kwenye mikoa," alisema.

Rais alisema fedha nyingi zimekuwa zikitoka wizarani kwenda mikoani lakini utekelezaji kwenye mikoa unasuasua na kuelekeza walioshindwa kuleta maji na kutumia fedha nyingi, wanapaswa wakae kando. "Wakae kando kupisha damu mpya ili wananchi wapate maji kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini ifikapo 2025," aliagiza.

Rais Samia alimwagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kuhakikisha kauli yake ya 'ukinizingua tutazinguana' inafanya kazi vinginevyo itarudi kwake.

"Tunakwenda kutunisha mfuko wa miradi ya maji, tunakwenda kuangalia vyanzo vingine vitakavyokwenda kutunisha Mfuko wa Maji ili tutekeleze upelekaji wa maji kwa wananchi haraka.

"Tunakwenda kuondoa utendaji mbovu na kuweka utendaji mpya na hapo hapo tukishindwa, Waziri wa Maji kabla ya kusema mimi, itabidi uondoke mwenyewe," alionya.

**GESI ASILIA**

Kuhusu kutelekezwa kwa mradi wa gesi asilia, Rais Samia alisema mazungumzo yake yamechukua miaka sita na sasa wanakwenda kuyamaliza na kutekeleza mradi.

Alisema serikali pia itatekeleza miradi ya nishati jadidifu itokanayo na jua, upepo na joto ardhi na katika miaka mitano, inatarajiwa kuzalisha megawati 1,000 kupitia vyanzo hivyo. Rais Samia pia alisema serikali inatarajia kuanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwamo ya bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Bandari ya Tanga lenye urefu wa kilometa 1,445 pamoja na Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG) mkoani Lindi.



## ATCL kufumuliwa kulelewa kimkakati

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema hasara ya uendeshaji inayoripotiwa katika Shirika la Ndege (ATCL), imetokana na madeni makubwa yaliyokuwapo awali.

Amesema serikali yake itachukua hatua kutua mzigo mkubwa unaolikabili shirika hilo ambalo kwa sasa linajiendesha kwa hasara inayotokana na kurithi madeni.

"ATCL litaendelea kulelewa na serikali kimkakati, ili kujiendesha kwa ufanisi. Hivi sasa linaonekana halina thamani, hii inatokana na kurithi madeni makubwa.

"Sote tunajua biashara ya ndege ni ngumu duniani, hatutakubali kuona hasara inaendelea baada ya kufanya uwekezaji, tutawekeza rasilimali watu wenye uwezo pamoja na kufanya uchambuzi wa kina. Sasa tutatumia wafanyakazi wenye weledi," alisema.

Kuhusu Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Rais Samia alisema ili kuongeza wigo wa usafirishaji mizigo, kuna haja kuiboresha na kupanua bandari zote na viwanja vya ndege ambavyo baadhi vimekwishafanyiwa maboresho.

SEKTA YA UTALII

Rais Samia alisema katika miaka mitano ijayo, serikali imejipanga kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni tano mwaka 2025 na mapato kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 za sasa hadi Dola za Marekani bilioni sita.

"Pamoja na uwapo wa janga la corona, katika miaka mitano ijayo, tunalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuongeza idadi ya watalii.

"Hatua tutakazochukua ni pamoja na kupanua wigo wa vivutio vya utalii, ikiwamo kukuza utalii wa mikutano, malikale na fukwe," alisema.

Alibainisha kuwa serikali ya awamu ya sita inakusudia kujenga miundombinu ya kuwezesha meli za utalii kuzuru nchini na kuhamasisha wawekezaji kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii hasa hoteli ili kupunguza gharama za malazi.

"Tunajipanga kusomesha vijana wengi katika taaluma ya utalii ili waendeshe maeneo mbalimbali ya sekta hiyo bila kutegemea wataalamu kutoka nje," alisema.

Alisema sekta hiyo imeajiri takriban watu milioni nne ambapo kwa miaka mitano iliyopita, ilikua kwa kiwango cha kuridhisha.

Rais Samia alisema idadi ya watalii waliotembelea nchini, iliongezeka kutoka watalii milioni 1.1 mwaka 2015 hadi watalii milioni 1.5 mwaka 2019 huku mapato yakiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.9 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019.

*Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA) na Christina Mwakangale (DAR)

# Nguvu kubwa kuelekezwa kukuza uchumi wa taifa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali inakusudia kuelekeza nguvu kubwa katika ukuzaji wa uchumi wa taifa.

Akilihutubia Bunge jana, Rais Samia alisema kwenye miaka mitano iliyopita taifa ilipata mafanikio ya kiuchumi kwa kusimamia ukuaji uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka.

Alisema serikali imedhibiti mfumuko wa bei kwa wastani wa asilimia 4.4 na kupunguza umaskini hadi asilimia 26.6.

"Muhimu zaidi mwaka jana mwezi Julai taifa liliingia kwenye kundi la uchumi wa kati ambapo pato la wastani kwa kila Mtanzania limeongezeka hadi Dola za Marekani 1,800, zaidi ya kigezo cha Dola za Marekani 1,036 za kuingia kwenye kundi hilo. Haya ni mafanikio makubwa," alisema.

Rais Samia alisema pamoja na mafanikio hayo, jitihada zinahitajika za kukuza uchumi, kupambana na umaskini kwa sababu kasi ya ukuaji uchumi ni ndogo.

"Wataalamu wa uchumi wanatueleza kwamba ukuaji wa uchumi na kupambana na umaskini, unatakiwa ukue angalau kwa asilimia nane kwa mwaka," alisema.

Alisema kutokana na dunia kukumbwa na janga la corona, kiuhalisia takwimu zinaonyesha uchumi wa nchi nyingi duniani umeshuka.

"Tanzania nayo imeathirika kwa kushuka kwa kiwango cha uchumi kutoka wastani wa asilimia 6.9 hadi 4.7, hii inamaanisha kwamba katika miaka mitano ijayo, unahitajika uwekezaji mkubwa, katika sekta za uzalishaji na zinazotoa ajira kwa wingi," alisema.

Rais Samia alitaja hatua zitakazochukuliwa katika kuhakikisha taifa linakuza uwekezaji ni kufanya marekebisho kadhaa katika sera, sheria na kanuni na kuondoa vifungu vinavyosababisha vikwazo katika kukuza sekta hiyo.

"Tutaendelea kuboresha sera zetu za uchumi wa jumla pamoja na sera za fedha na kuhakikisha viashiria vyote vya uchumi, ikiwamo thamani ya sarafu yetu, mfumuko wa bei na viwango vya riba, vinabaki kwenye hali ya utulivu," alisema.

Alisema watachukua hatua madhubuti kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuivutia sekta binafsi kushiriki vizuri kwenye shughuli za kiuchumi.

"Mwelekeo utakuwa ni kurudisha imani ya wawekezaji, na kutoa vivutio kwa wawekezaji mahiri ikiwa ni pamoja na kuwezesha uwekezaji kufanyika kwa haraka, kumekuwa na mzunguko mkubwa watu wanapotaka kuja kuwekeza.

Rais Samia alisema suala la upatikanaji wa mitaji halinabudi kuangaliwa kwa umakini mkubwa kwa sababu ili sekta binafsi ishiriki vizuri, hawanabudi kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

"Nchi yetu imekuwa ikilalamikiwa kwa kutokuwa na mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ikiwamo kutokuwa na sera zinazotabirika, utaratibu wa kodi usio na utulivu, urasimu mwingi katika kutoa huduma za uwekezaji na mengine yanayokwamisha ustawi wa biashara," alisema.

Alisema wanakusudia kufanya maboresho makubwa kwenye eneo hilo kwa kuhakikisha wanatekeleza kikamilifu mpango wa kuboresha mazingira ya biashara.

Rais Samia alisema urasimu unajumuisha pia ucheleweshaji wa kutoa vibali vya biashara na leseni na kuagiza lifanyike kwa muda mfupi na suala la upatikanaji wa ardhi nalo liwekwe sawa.



Viongozi wakuu wastaafu wakifuatilia hotuba ya Rais, Samia Suluhu Hassan, Bungeni jijini Dodoma jana.

# ... Kilimo, mifugo, uvuvi kupewa kipaumbele

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

RAIS Samia amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo serikali yake itajikita katika kuinua na kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Akihutubia Bunge jijini Dodoma jana, alisema kutafanyika jitihada za kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kwa wakulima, taasisi za kilimo kupewa mitaji ili ziweze kuzalisha mbegu bora. Serikali pia itatumia wataalamu wa ndani kuzalisha mbegu, kukuza utafiti, maofisa ugani, pamoja na kuuza mazao nje ya nchi.

Kadhalika, kukuza na kuendeleza sekta ya umwagiliaji kwa wakulima na kuanza kuchangia katika mfumo huo. Nguvu zaidi zitaelekezwa katika ujenzi wa vihenge na maghala ili kuzuia upotevu wa mazao. "Zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima, lakini mchango katika pato la taifa ni asilimia 27 tu, bado inakabiliwa na matatizo mengi. Uzalishaji bado ni mdogo kwa mfano kwenye zao la mahindi badala ya kuzalisha tani nane kwa hekta sisi tunazalisha tani moja," alisema Rais Samia.

Alisema serikali itajielekeza katika kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili iweze kutoa mikopo kwa wakulima. Pia bima ya kilimo itawekewa misingi imara.

MIFUGO

Rais Samia alisema katika miaka mitano ijayo serikali itajielekeza katika ufugaji wa kisasa, kuongeza mbegu bora, maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni mbili hadi milioni sita, lengo kuu likiwa ni kupunguza ufugaji wa kuhamahama.

"Tuna mbinu ndogo za ufugaji, ng'ombe wetu wanatoa maziwa lita tatu Kwa siku badala ya 20. Tunazalisha kilo 150 za nyama badala ya 500 hadi 600 kama walivyo wenzetu," alisema Rais Samia.

UVUVI

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali itanunua meli mpya nane za uvuvi, zitakazofanya uvuvi katika bahari kuu. Kati ya meli hizo, nne zitakuwa Zanzibar na nne Tanzania Bara Rais Samia alisema kutajengwa bandari, vizimba vya uvuvi wa samaki, pamoja na viwanda vya kuchakata samaki.

MADINI

Serikali katika miaka mitano ijayo itajielekeza katika kusimamia sheria ya madini ya mwaka 2017, kuzuia utoroshaji na kuvutia wawekezaji. Pia kutawekwa msukumo kwenye kusimamia masoko ya madini, viwanda kuwa na teknolojia bora, kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwapa mikopo na elimu.

Kadhalika Shirika la Madini (STAMICO), lengo kuu ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 sekta ya madini ichangie asilimia 10 katika pato la taifa.

Sekta ya madini mchango wake katika pato la taifa ni mdogo, mwaka 2015 ilichangia asilimia 3.4, mwaka 2019 ilichangia asilimia 5.2, mwaka 2015 makusanyo ilikuwa Sh. bilioni 168, mwaka 2020 ilikuwa Sh. bilioni 527," alisema Rais Samia.

# Serikali yatangaza neema ajira mpya 44,000

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amesema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,096.

Kati yao, kada ya elimu ni 10,297, afya 11,215, kilimo 1,383, mifugo 1,250, uvuvi 733, Jeshi la Polisi 1,782, Magereza 843, Jeshi la Zimamoto na Uhamiaji 512 na hospitali za mashirika ya kidini na hiari 1,240.

Aliyasema hayo jana bungeni alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha (2021/22).

Akiwasilisha makadirio hayo, Mchengerwa alisema serikali pia itaajiri watumishi 14,841 wa kada mbalimbali ikiwamo wahadhiri wa vyuo vikuu vyote vya umma nchini pamoja na kada nyingine ambazo haziko kwenye sekta zilizoainishwa.

Waziri huyo alisema katika mwaka 2021/22, watumishi 92,619 wa kada mbalimbali watapandishwa vyeo na watumishi 2,360 watabadilishwa kada katika utumishi kulingana na maelekezo yatakayotolewa wakati huo.

Mchengerwa alisema: "Pia kutafanyika uchambuaji na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma wapatao 17,699 yenye thamani ya Sh. bilioni 37.474 na kuchukua hatua ipasavyo".

Alisema serikali pia itaimarisha mifumo na uwezo wa matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumishi kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo haki zao na ya wananchi kuhusu huduma za utumishi wa umma kwenye ngazi zote, ili kupunguza kwa kiwango kikubwa kero hizo.

"Ninatoa rai kwa maofisa utumishi wote kushughulikia changamoto zote za watumishi haraka. Ninarudia kusisitiza kuwa tukitembelea kwa mwajiri yeyote tukakuta malalamiko yanayoweza kutatuliwa na mwajiri, tutachukua hatua kali, ikiwamo kuwavua madaraka waliozembea.

"Pia, ninawaomba wabunge kuleta kero na malalamiko ya watumishi wa umma kutoka katika majimbo yenu moja kwa moja kwangu wakati wowote. Nimedhamiria kupunguza kama siyo kumaliza kabisa malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi yanayohusu ofisi yangu," alisema.

Mchengerwa alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, serikali itafanya ukaguzi na kuidhinisha watumishi wapya wanaostahili kuingizwa katika orodha ya malipo ya mishahara.

Alisema pia kutafanyika uidhinishaji wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na malipo ya mishahara katika utumishi wa umma.

Waziri huyo alisema wizara itatoa vibali vya ajira mpya na mbadala ili kujaza nafasi stahiki kwenye taasisi mbalimbali za umma, kufanya uhakiki wa watumishi, ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya rasilimaliwatu sambamba na kusafisha na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia Mfumo wa HCMIS.

"Mwaka ujao tutaziwezesha wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali na mashirika ya umma 20 kuandaa orodha ya kazi na maelezo ya kazi, ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya taasisi husika," alisema.

# Wabunge waonywa matumizi ya mtandao

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SIKU moja baada ya Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, kuliwasilisha bungeni suala la mitandao ya kijamii kuwekwa taarifa za kuhatarisha amani ya nchi zikiwahusisha baadhi ya viongozi wastaafu, Spika wa Bunge, Job Ndugai, amewatahadharisha wabunge kuhusu taarifa za kwenye mitandao hiyo.

Amewataka watunga sheria hao kuitumia mitandao ya kijamii kama rejea bungeni, lakini kwa tahadhari na uangalifu mkubwa.

Juzi, Sanga, akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alisema tangu kutokea kwa kifo cha Rais John Magufuli, kumeibuka wimbi la watumiaji wa mitandao ya kijamii wakiwasema vibaya viongozi wastaafu, jambo linalohatarisha usalama wa nchi.

Mbunge huyo aliwataja viongozi hao kuwa ni pamoja na Rais mstaafu Jakaya Kikwete, Katibu Mkuu wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana. Wengine ni Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye na Spika Ndugai.

Alisema hatua ya kuwasema vibaya viongozi hao ni hatari kwa taifa na kwamba serikali inapaswa kukomesha tabia hiyo.

Hoja hiyo ilimwinua kwenye kiti Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kirumbe Ng'enda, aliyesimama na kuomba mwongozo wa Spika, akitaka kufahamu kama taarifa za mitandao ya kijamii zinaruhusiwa kununukuliwa kama rejea bungeni.

Akijibu mwongozo huo jana, Spika Ndugai alisema: "Mitandao ya kijamii tuitumie kwa reference (rejea), lakini kwa tahadhari na uangalifu mkubwa sana hususani katika majadiliano hapa bungeni."

"Mheshimiwa mbunge usifanye rejea ya taarifa hizo bila ya kufanya kwanza udhibitisho na utafiti zaidi wa ukweli wake. Kanuni zetu zinazuia mbunge kutoa taarifa za uongo bungeni.

"Endapo mbunge akitoa taarifa hizo, atatakiwa kudhibitisha ukweli wa taarifa hizo. Utalazimika kufanya hivyo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

"Utakapotakiwa kufanya hivyo kwa rejea zako za mitandao ya kijamii, na utakuwa huna ushahidi, utajikuta unaingia katika matatizo. Huo ndiyo mwongozo wangu."


## CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

# TANGAZO

## MAFUNZO YA UONGOZI NA MAADILI

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), kinapenda kuwatangazia kuwa kutakuwa na Mafunzo maalumu ya Uongozi na Maadili yatakayofanyika kwa muda wa wiki moja. Lengo la Mafunzo haya ni kuwajengea uwezo washiriki katika stadi za Uongozi, Maadili na utawala bora na kuwajenga katika misingi imara ya Uongozi bora, uwajibikaji na uzalendo katika taasisi zao za Umma na binafsi kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

**Malengo mahususi ya Mafunzo**

i. Kujenga uelewa wa nadharia ya maadili na utawala bora na misingi ya utumiaji wa uelewa huo katika maeneo ya kazi.
ii. Kuboresha weledi wa washiriki katika kutatua migogoro na kufanya makubaliano ya kidiplomasia sehemu za kazi.
iii. Kuendeleza uwezo wa kufanya maamuzi kama viongozi na kupanua kiwango cha uelewa wa maadili na utawala bora kwa Washiriki.

**Walengwa**

Viongozi, Viongozi tarajali pamoja na Watumishi walio katika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi katika taasisi za umma na binafsi.

**Muda wa Masomo**

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa wiki moja ambapo Mshiriki atachagua awamu moja kati ya nne kama ifuatavyo:

| Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Mahali | Cheti kitakachotolewa |
|---|---|---|---|
| 3/5/2021 | 7/5/2021 | Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 2/8/2021 | 6/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 23/8/2021 | 27/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 6/9/2021 | 10/9/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi |

**Ada ya Mafunzo**

Gharama ya Mafunzo haya ni TZS 500,000/ ambayo italipwa kabla ya Mafunzo kuanza. Baada ya malipo, fedha haitaweza kurejeshwa.

**Jinsi ya kutuma maombi**

Maombi kwa ajili ya kuhudhuria Mafunzo haya yako wazi kuanzia sasa.
Mwombaji atatuma maombi yake kwa njia ya mtandao kwa kujaza fomu iliyokatika tovuti ya Chuo ambayo ni: www.mnma.ac.tz.
Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya Mafunzo haya itakuwa ni wiki moja kabla ya tarehe husika ya kuanza kwa mafunzo.

**Mawasiliano**

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu programu hii maalumu ya Uongozi na Maadili unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Mafunzo ya Uongozi na Maadili kupitia namba ya simu ya mkononi 255(22)2820041/47 au +255675337734: email: phillip.daninga@mnma.ac.tz au rector@mnma.ac.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkuu wa Chuo**
**Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ijipange kwa ongezeko wanafunzi

**TOLEO** letu la jana nilikuwa na ripoti iliyoangazia kasi ya ongezeko la wanafunzi iliyochagizwa na kuanza kutekelezwa kwa Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo, maarufu elimu bure.

Tathmini na ripoti mbalimbali za kiukaguzi zikiwamo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinaonyesha kuwa mwakani kutakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliodahiliwa kujiunga darasa la kwanza kwa mpango wa elimu bure watakaojiunga na kidato cha kwanza.

CAG ameshanyooshea kidole suala hilo, akiitaka serikali kujipanga kukabiliana na 'mlipuko' huo ambao maandalizi yake ya kina yanapaswa kufanyika ndani ya miezi minane iliyobaki.

Mkaguzi Mkuu huyo ameshabainisha kwamba udahili wa wanafunzi katika shule za msingi nchini uliongezeka kutoka wanafunzi milioni 4.8 mwaka 2001 hadi milioni 8.34 mwaka 2016, yaani katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango wa elimu bure.

Katika miaka hiyo minne iliyopita, mkaguzi hiyo wa kitaifa aliainisha idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi nchini ilikuwa milioni 8.34 kwa shule za serikali na madarasa yao yalikuwa 108,448, ambayo ni wastani wa nusu (asilimia 52) ya mahitaji halisi ambayo ni madarasa 208,540.

Pia, kwa kutumia kigezo hicho, inamaanisha kulikuwa na ukiukwaji wa kanuni za ufundishaji bora, unaohitaji darasa liwe na wanafunzi wasiozidi 45, lakini kulinganisha na hali ilivyokuwa, darasa moja lilisheheni wanafunzi 77, ambayo inakaribia kuwa sawa na madarasa mawili.

Kwa mantiki hiyo, wakati mwaka 2016 kulivyoshuhudiwa mlipuko wa udahili ambao ulielemea uhalisia wa mahitaji kutokana na serikali kuanza kudahili pasipo malipo (elimu bure), tayari miaka kadhaa kabla, jahazi hilo lilikuwa limeanza kuelemewa.

Ndani ya mtazamo wa ubashiri kama wa CAG, tathmini iliyofanywa na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na kongani ya elimu, zinaonyesha katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, idadi ya wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza itaongezeka hadi kufikia wanafunzi 1,882,500, ikiwa ni takriban mara mbili ya takwimu za mwaka 2015.

Nipashe tunaishauri serikali kuhakikisha ongezeko hilo la wanafunzi liende sambamba na mahitaji ya madarasa, walimu, vitabu, vyoo na ruzuku ya elimu bure.


Tathmini za kitaalamu kuhusu kasi ya ongezeko hilo zinaonyesha kuwa kutokana na idadi hiyo ya wanafunzi, kutahitajika madarasa 41,833, sasa kukiripotiwa kuwapo uhaba wa madarasa 4,647 katika shule za sekondari nchini, hivyo kufanya uhitaji uwe mkubwa zaidi kufikia madarasa 46,480.

Nipashe pia tunaishauri serikali kujipanga kuongeza matundu ya vyoo 75,000 yatayohitajika, vitabu milioni 18.825, walimu 41,833 na Sh. bilioni 47 kila mwezi kwa ajili ya ruzuku ya elimu bure.

Tunaamini kuwa, bila kuwapo mkakati kitaifa kukabiliana kasi ya ongezeko la wanafunzi iliyopo, CAG akibainisha kuwapo ongezeko la asilimia tano kwa mwaka, wanafunzi wengi walioanza darasa la kwanza mwaka 2016, hawatapata nafasi kujiunga na kidato cha kwanza mwakani kutokana na uhaba wa miundombinu.

Shime, serikali ichukue hatua kukabiliana na ongezeko hili kwa kuboresha miundombinu ya shule iliyopo, kujenga shule mpya na kuajiri walimu wapya ili kukidhi mahitaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Lami muhimu barabara itokayo Nangurukuru kuikomboa Liwale

**KWA** aliyewahi kusafiri kutoka Nangurukuru hadi Liwale kupitia Kilwa Njinjo mkoani Lindi, kipindi cha mvua, ni wazi anajua adha ya kukwama njiani kwa muda mrefu, kutokana na barabara kujaa matope.

Ni barabara kongwe umbali kilomita 230, inayotegemewa na wasafirishaji wa abiria, mazao na biashara mbalimbali wakiwamo mifugo.

Wilaya ya Liwale, ni miongoni mwa maeneo ambayo watu wanaotoka mikoa mbalimbali wamewekeza.Mahali hapo, pamekusanya watu kutoka karibu kila kona ya nchi, wanaojishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali, biashara kama maduka, bucha na wafugaji wa ng'ombe.

Wote hao wanategemea barabara hiyo wanapohitaji kusafirisha biashara zao, kwenda katika masoko kama vile jijini Dar es Salaam, lakini wakati wa mvua mustakabali huo unakuwa mtihani kwa kuwa barabara hiyo huwa haipitiki.

Kwa wale waliozoea kuona ng'ombe wa kuchinjwa wakitolewa mkoani Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na Mwanza kupelekwa jijini Dar es Salaam, nawajulisha kuwa siku hizi ng'ombe wengine wanatoka Liwale.

Hatua hiyo inaonyesha kuwa mambo yamebadilika kwa kuwa hata maeneo ya Kilwa na Liwale, kuna ng'ombe ambao husafirishwa na kupelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya kuchinjwa.

Kikwazo kikubwa cha kufikisha mifugo hao kwa wakati, ni barabara kutojengwa kwa kiwango cha lami, hali inaweza kukwamisha maendeleo ya wafanyabiashara na wilaya kwa ujumla.

Hata hivyo, kuna bahari njema iliyotangazwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa, kwamba kuna pesa Sh. bilioni 1.3 zimetolewa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara hiyo.

Akiwa katika mkutano wa kampeni za uchaguzi Kata za Likongowele, wilayani Liwale kwenye Uwanja wa Ujenzi ni kwamba ujenzi wa barabara hiyo umo katika hisani ya mpango wa mwaka 2020/2025, kqwa mujibu wa Ilani ya chama tawala CCM.

Hiyo ni habari njema kwa wakazi na wafanyabiashara wa maeneo hayo hasa itakapotimia kuwa itawaondolea kero ya muda mrefu iliyokuwapo tangu Liwale kutengwa kuwa wilaya mwaka 1975.

Ni ahadi inanyoonyesha kilio chao kimesikika, hivyo itapendeza kama itatimia ili kusaidia kuboresha biashara za huko, zikiwamo za kusafirisha ng'ombe wa kuchinjwa kwenda Dar es Salaam.

Umuhimu wa barabara hiyo si tu kwa watu wa maeneo hayo, bali pia kwa maendeleo ya Mkoa wa Lindi na nchi kwa ujumla, hivyo inapendeza kama ingetengezwa ili ipitike kipindi chote.

Kwa wakati huu ambao mvua zimeanza kunyesha, ninaamini kwamba watumiaji barabara hiyo, wakiwamo wafanyabishara, watakuwa wameanza kutafakari kero wanayoipata kila msimu wa mvua.

Niseme, ubora wa barabara hiyo utasaidia Liwale kufunguka kibiashara na kiuchumi na kujiimarisha katika mtandao wa barabara zitakazoiunganisha wilaya hiyo na wilaya jirani na nchi kwa ujumla.

Suala la uboreshaji miundombinu ya barabara hiyo, imekuwa kilio cha muda mrefu katika wilaya hiyo, kutokana na kwamba katika kipindi cha mvua, watu huanza kuwaza jinsi ya kusafiri, hasa wanaoelekea jijini Dar es Salaam.

Barabara hiyo inaposhindikana kupitika, watu wanalazimika kuzunguka Nachingwea hadi Masasi mkoani Mtwara kuelekea Dar es Salaam, mwendo ambao ni zaidi ya kilometa 230 za kupitia Njinjo.

Naamini barabara hiyo ikijengwa kwa kiwango cha lami, itapunguza kero hiyo na kufanya Liwale na mkoa wa Lindi kwa ujumla kuaendelea kiuchumi, kutokana na ukweli wilaya hiyo ina fursa lukuki za biashara ambazo hazitatumika kwa kina.

Hadi sasa Liwale bado ni kisiwa katika msimu wa mvua , kwa kuwa haina hata barabara ya lami inayoingia wilayani humo, kwani hata ya kutoka Nachingwe kuingia wilayani humo, yenye urefu wa kilometa 129, nayo haina lami.

# ATE kupendekeza majina ya wanawake serikalini kwa uteuzi

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimesema hivi karibuni kitaikabidhi serikali takwimu za wanawake waliopata mafunzo ya 'Mwanamke Kiongozi' ili nafasi za uteuzi kwenye bodi mbalimbali zinapotokea wateuliwe.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa chama hicho, Dk. Aggrey Mlimuka, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya awamu ya saba yanayotolewa kwa wanawake walio kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa lengo la kuwawezesha kuteuliwa kuingia kwenye bodi na kushiriki katika kutoa uamuzi.

Akizungumza katika mafunzo hayo ambayo yamewaleta pamoja jumla ya wanawake 35 katika awamu hiyo, alisema mpaka sasa tangu yazinduliwe mwaka 2016, wahitimu ni 150.

"Mwisho wa mwaka huu tutakuwa na wanawake 180 waliopata mafunzo haya, hakuna sababu ya mawaziri kusema sina wanawake wa kuteua. Tumekuwa tukiyatoa mafunzo haya kwa miezi tisa.

"Takwimu za waliopata mafunzo tutazikamilisha na zitapelekewa serikalini ili mawaziri wasiwe na sababu ya kusema katika nafasi za uteuzi hatuna wanawake wa kuwateua kwenye bodi," alisema.

Dk. Mlimuka aliwataka wote waliopata mafunzo hayo wanapopata nafasi hizo wafanya kazi ili wasinyooshewe vidole.

"Kwa umri wangu uzoefu unaonyesha bodi ambazo zipo chini ya wanawake zinafanya vizuri kuliko zenye wanaume wengi, wanawake hawakubali kuhongwa kirahisi, msiwaangushe waliowatangulia ambao wameweka viwango vya juu vya kiuongozi kwa kufanya vizuri," alisema.

Alisema mafunzo hayo yanawaandaa kushika madaraka kwa kufundishwa masuala ya uongozi, kujenga hoja na kutokuwa na woga wa kuzungumza kwenye hadhara na wanafundishwa namna ya kuandaa hotuba.

Mkurugenzi Rasilimali Watu kutoka benki ya CRDB, Siaophoro Kishimbo, alitoa mfano kwenye benki katika nafasi za Maofisa Watendaji Wakuu (CEO) wanawake waliopo ni wawili pekee ambao ni viongozi wa benki kubwa Tanzania namba ambayo bado ni ndogo.

"Hili ni tatizo tunahitaji kuongeza juhudi zaidi katika kuwawezesha wanawake kwa mafunzo kama haya ili waweze kuchukua nafasi za juu," alisema.

Naye, Mkufunzi wa Chuo cha Uongozi cha Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI) jijini Arusha, Prof. Apollonia Kerenge, alisema lazima mwanamke awe na mkakati wake na aongee na familia.

"Wengi tumeanza kukubali uongozi wa mwanamke ambao umefanyiwa utafiti na kuonyesha wanawake ni viongozi bora, lakini siyo kwamba watakupa cheo kwa sababu wewe ni mwanamke lazima uonyeshe unaweza," alisema.

# Bil. 400/- zatumika kukabili malaria

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani nchini umebainisha kuwa nchi hiyo imewekeza Dola za Marekani milioni 176 (Sh. bilioni 406.294) kupambana na malaria nchini katika miaka minne iliyopita.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na ubalozi huo, ilibainisha kuwa mwaka jana, ugonjwa wa corona ulisababisha janga la kidunia ambalo halikutegemewa kutokea.

Hata hivyo, ubalozi huo ukasisitiza kuwa malaria imekuwa tatizo kwa muda mrefu nchini na Marekani inajivunia kuisaidia Tanzania kuendelea na mapambano yake dhidi ya malaria.

Ubalozi huo ulibainisha kuwa jitihada ambazo Tanzania imechukua kuendeleza huduma muhimu za malaria, zinaokoa maisha ya watu wengi.

Katika taarifa yake hiyo, ubalozi huo ulibainisha kuwa Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) umeshirikiana na Tanzania kupambana na malaria tangu 2006 na kuchangia Dola za Marekani milioni 176 katika miaka minne iliyopita.

Ulisema kuwa ufadhili huu umewasilisha vyandarua vyenye viatilifu, dawa za kuokoa maisha, upimaji wa kiwango cha juu na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya zaidi ya 4,700 hadi sasa.

Kupitia ushirikiano wa karibu na watu, taasisi na serikali ya Tanzania, ubalozi huo ulisema Serikali ya Marekani pia inaimarisha mifumo ya afya na kuongeza juhudi za Tanzania kumaliza ugonjwa huo hatari.

"Maendeleo makubwa ya Tanzania dhidi ya malaria yameangaziwa katika Ripoti ya 15 ya Mwaka ya Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria. Kwa mfano, umiliki wa vyandarua vyenye viatilifu umeongezeka hadi asilimia 78 kutoka asilimia 23 mwaka 2005.

"Kulala kwenye vyandarua vyenye viatilifu huzuia mbu wakati wa usiku, wakati wana nafasi kubwa ya kuuma na kuua mbu wanaotua kwenye chandarua. Hivyo, kupunguza kuenea kwa malaria," ilibainisha taarifa hiyo.

Wakati wa mahojiano ya hivi karibuni na kituo kimoja cha redio jijini Dar es Salaam kuadhimisha Siku ya Malaria Duniani, Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Andrew Karas, alisema uwekezaji wa PMI unasaidia na kujenga juu ya yale mambo muhimu yaliyofanywa na Serikali ya Tanzania.

"Ufadhili wetu unalingana na vipaumbele vya Tanzania vilivyoainishwa katika Dira yake 2025 yenye kuzingatia kuendeleza watendaji wa kazi, na pia taasisi na mifumo ambayo serikali inaona ni muhimu kufikia na kudumisha dira yake ya muda mrefu," ubalozi huo ulibainisha zaidi katika taarifa hiyo.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)**
**Dar es Salaam, Aprili 08, 2021**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz

# TANGAZO

BancABC part of atlasmara

## AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,013 | 3,289 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,430 | 7,028 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 44,150 | 43,178 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,830 | 3,915 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 104,467 | 108,008 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 130,214 | 133,952 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 26,974 | 27,803 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,231 | 6,583 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **331,310** | **334,756** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 104,164 | 106,624 |
| 18 | Amana za Wateja | 111,016 | 111,082 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,842 | 3,014 |
| 28 | Madeni | 75,705 | 74,640 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **292,727** | **295,360** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **38,584** | **39,396** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,705 | 2,705 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (86,263) | (82,111) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (812) - | 4,152 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,584** | **39,396** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 2,618 | 2,866 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 21,126 | 19,585 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,127 | 15,128 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.65% | 11.77% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.54% | 13.14% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.54% | 68.48% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39.30% | 44.53% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 47.89% | 48.30% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.16% | 12.18% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.03% | -3.56% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,133 | 10,245 | 10,133 | 10,245 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,832) | (4,751) | (4,832) | (4,751) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,301** | **5,494** | **5,301** | **5,494** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 77 | 182 | 77 | 182 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,251** | **1,073** | **1,251** | **1,073** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 292 | 479 | 292 | 479 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 200 | 180 | 200 | 180 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 760 | 413 | 760 | 413 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,349)** | **(7,348)** | **(7,349)** | **(7,348)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,575) | (2,536) | (2,575) | (2,536) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,775) | (4,812) | (4,775) | (4,812) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(719)** | **(599)** | **(719)** | **(599)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (93) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(812)** | **(633)** | **(812)** | **(633)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(812)** | **(633)** | **(812)** | **(633)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 142 | 151 | 142 | 151 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.33) | (0.26) | (0.08) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 7 | 6 | 7 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.98% | -0.81% | -0.98% | -0.81% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -8.33% | -5.85% | -8.33% | -5.85% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 112.15% | 111.90% | 112.15% | 111.90% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.95% | 3.37% | 2.95% | 3.37% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (719) | (4,006) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 886 | 5,380 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,738 | (8,017) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,527) | 26,044 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (972) | (10,127) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,171) | (1,395) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 829 | (746) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (93) | (135) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(30)** | **6,998** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (534) | (4,046) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(534)** | **(4,046)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,065 | 5,088 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,065** | **5,088** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 501 | 8,040 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 122,240 | 114,200 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **122,741** | **122,240** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2021
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(86,820)** | **2,274** | **-** | **989** | **39,396** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (812) | - | - | - | **(812)** |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(87,633)** | **2,274** | **-** | **989** | **38,584** |
| | - | - | - | - | - | - | **0** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130.00** | **-** | **1,065** | **43,623** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (4,152) | - | - | - | **(4,152)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (2,144) | 2,144 | - | (76) | **(76)** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(86,820)** | **2,274** | **0** | **989** | **39,396** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 22nd April 2021 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 22nd April 2021 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 22nd April 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 22nd April 2021 |
| Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 22nd April 2021 |

# Hati yenye shaka yamtia matatani mweka hazina

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, limeazimia kusimamishwa kazi mweka hazina wa halmashauri hiyo, Deus Ngelanizya, kwa kushindwa kudhibiti na kusimamia mapato ya serikali. Amesimamishwa ili kupisha uchunguzi dhidi yake kwa tuhuma za kuisababishia halmashauri hiyo kupata hati yenye shaka.

Maazimio hayo yalitolewa juzi kwenye baraza hilo wilayani Kishapu, wakati wakijadili ajenda mbalimbali za maendeleo ya wilaya hiyo, ikiwamo kujitathmini baada ya kupata hati yenye shaka.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Williamu Jijimya, akitangaza maazimio ya baraza hilo, alisema mweka hazina huyo ndiye chanzo cha wao kupata hati yenye shaka, kutokana na kudharau maagizo ya madiwani, na kushindwa kudhibiti mapato na kuwasababishia kuingia kwenye kumbukumbu mbaya.

“Tumeazimia mweka hazina, achukuliwe hatua ya kusimamishwa kazi, ili kupisha uchunguzi wa kushindwa kusimamia vyema mapato ya Halmashauri na kutusababishia kupata hati yenye shaka pamoja na kuwa wa mwisho kitaifa kwenye makusanyo ya nusu mwaka 2020/2021,” alisema Jijimya.

“Mweka hazina huyu amekuwa akidharau sana maagizo ya baraza la madiwani, tulishamwagiza asimamie vizuri fedha za mapato ya halmashauri na fedha za madeni pamoja na kuziweka benki kwa wakati, lakini hakufanya hivyo na sasa tumeingia kwenye hati ya shaka, lazima awajibishwe,” aliongeza.

Naye Katibu Tawala wilaya ya Kishapu, Shandrack Kengese, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa wilaya hiyo, Nyabaganga Talaba, aliitaka Halmashauri hiyo ijitathmini kwenye suala la ukusanyaji mapato na kuyadhibiti, ambayo ndiyo nguzo ya maendeleo pamoja na kuibua vyanzo vipya.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Emmanuel Johnson, aliitaka idara ya fedha kujitathmini juu ya utendaji wao kazi, pamoja na kumwandalia taarifa ya fedha na kuiwasilisha ofisini kwake Jumatatu ijayo.




Mhifahi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Siha, Innocent Chegenda (kulia), akikabidhi moja ya miche ya miti 10,000 kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Mainoya, kwaajili ya utekelezaji wa kampeni ya ‘Tigo Green for Kili’, wilayani humo mkoani Kilimanjaro jana, yenye lengo la kurejesha hadhi ya theluji ya Mlima Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana, wakulima kunufaika kwa ufadhili wa SBL

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya bia ya Serengeti Breweries Limited (SBL) imesema imedhamiria kuendelea kutengeneza maisha bora kwa vijana na wakulima nchini kupitia programu yake ya udhamini wa masomo kwa wanafunzi wanaotoka familia masikini kwenye vyuo vinavyofundisha kilimo.

Programu hii iliyoanzishwa mwaka 2010, imesaidia wanafunzi 71 kusomea kozi za diploma katika ujuzi wa kilimo katika vyuo vinne kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa SBL, Mark Ocitti. Katika tukio la kuwapongeza wananfunzi 17 waliopata nafasi za ufadhili kupitia programu hii kutoka chuo cha Mt Maria Goretti Agriculture Training Institute, Ocitti alinukuliwa akisema kuwa Kilimo Viwanda imelenga kusaidia wanafunzi kutoka familia masikini ili waweze kusomea masomo ya kilimo kwenye ngazi ya diploma katika vyuo vya ndani.

Wanafunzi wengine 43 chini ya programu hii wanapatikana Kaole Wazazi College of Agriculture (Bagamoyo), Kilacha Agriculture and Livestock Training Institute (Moshi) na Igabiro Training Insitute of Agriculture (Bukoba).

Ocitti alifafanua kuwa ufadhili huu unajumuisha malipo yote ya chuo na gharama zingine katika kipindi chao chote cha masomo.

Vilevile, Viwanda inalenga kuongeza nguvu jitihada za Serikali katika kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuongeza idadi ya wataalamu wa mashamba watakaowasaidia wakulima kuboresha mashamba yao. SBL inategemea kwa kiasi kikubwa mazao ya nafaka kama vile mtama, shayiri na mahindi katika uzalishaji wao.

Vilevile Ocitti alisema: ‘Programu hii ni fursa nzuri kwa wanafunzi kuongeza upeo wao kwa kujifunza kimatendo watakapotembelea mashamba makubwa ya wakulima wanaolima nafaka kama hizi pamoja na kutembelea viwanda vyetu vya Dar es Salaam, Moshi na Mwanza ili kushuhudia namna kilimo na uzalishaji unavyotegemeana.”“Kwa sasa kampuni inafanya kazi na mtandao wa wakulima 400 kwenye mikoa nane nchini ambapo mwaka jana tulinunua nafaka tani 17,000 sawasawa na asilimia 70 na mahitaji yetu kwa mwaka. Tumedhamiria kuongeza ununuzi hadi kufikia asilimia 85 hadi kufikia 2025 ikiwa ni fursa adimu kwa wakulima wa ndani.”

Mkuu wa Chuo hicho, Isaya Marcus Kigava, aliipongeza na kuishukuru SBS kwa kusudi lao zuri la kuwasaidia wanafunzi hao katika kuboresha maisha yao ya baadae.

“Ni programu muhimu sana kuwapa elimu ya kimatendo ili waweze kufanya vyema kwenye kilimo cha biashara.”


BancABC part of atlasmara

**AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED**

**MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES**

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2,000,000.00 | $ 2,000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3,000,000.00 | $ 3,000.00 | £ 3,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | £ 1,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | £ 5,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4,000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40,000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50( | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2,500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6,000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5,000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

# Serikali yapata dawa uhaba mafuta ya kula

SERIKALI imesema itauwezesha Wakala wa Mbegu (ASA) Sh. bilioni 10.6 ili kuzalisha tani 5,000 za mbegu za alizeti kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini katika mwaka ujao wa fedha.

Vilevile, imesema Wizara ya Kilimo imeanzisha miradi ya 'block farming' katika mikoa ya uzalishaji mbegu za mafuta ikiwamo alizeti, michikichi na pamba.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Ditopile.

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kuwawezesha wakulima nchini kuwekeza katika kilimo cha mazao ya alizeti, michikichi na karanga ili kuokoa kiasi cha fedha kinachotumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi. Akijibu swali hilo, Bashe alisema kuwa katika mwaka ujao wa fedha, serikali itatoa kipaumbele kwa kilimo cha uzalishaji mbegu kwa mfumo wa 'block farming' kwenye baadhi ya mikoa kwa ajili ya uzalishaji mbegu za alizeti, pamba na michikichi.

Alibainisha kuwa mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa tani 570,000 kwa mwaka na uzalishaji wa mafuta ya kula nchini unakadiriwa kufikiwa wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka.

"Hali hii husababisha nchi kutumia wastani wa Sh. bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi kwa mwaka," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji kama serikali ina mpango wa kusitisha mfumo wa stakabadhi ghalani kwa baadhi ya mikoa ikiwamo Dodoma kutokana na kero kadhaa zilizopo au la.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema serikali itasitisha matumizi ya mfumo huo kwa mwaka mmoja katika mikoa mitano kutokana na tatizo la kutokuwapo kwa vyama vya ushirika imara.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Dodoma, Morogoro, Singida, Katavi na Songwe huku akiagiza mikoa hiyo kuanza kusajili wanunuzi wa mazao bila gharama huku wakizuia kutumia madebe katika ununuzi wa ufuta.

Bashe alisema mfumo huo utasitishwa kwa mwaka mmoja ili kuimarisha vyama vya ushirika kwa kuwa mfumo huo ni maelekezo yaliyo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema katika kukuza na kuimarisha masoko ya ufuta, choroko na dengu, aliwataka wakuu wa wilaya, mikoa na wakurugenzi kuzuia uuzaji wa mazao hayo kwa kutumia madebe.

Alisema hatua hiyo inatokana na kuwapunja wakulima na kutoa mfano wa debe la ufuta linauzwa kilo 14,000 kwa Sh. 20,000 wakati katika Bandari ya Dar es Salaam kilo moja ikiuzwa kwa Sh. 3,000.



Mbunge wa Kuteuliwa, Bashiru Ally (kulia) akiwa na Mbunge wa Makete, Festo Sanga, wakingia kuhudhuria vikao vya bunge la bajeti, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

## Alama 1,000 zawekwa mpaka Tanzania, Kenya

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeliambia Bunge kuwa hadi sasa, sehemu ya Mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa Km 172 kutoka Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron, imeimarishwa kwa kuwekewa alama 1,135.

Naibu Waziri, Dk. Angeline Mabula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Mkinga (CCM), Dunstan Kitandula.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuhakiki na kuweka alama kwenye Mpaka wa Tanzania na Kenya kwa eneo la nchi kavu na baharini ili wananchi wa mpakani wilayani Mkinga waondokane na kero ya muda mrefu ya kukamatwa na kutaifishiwa mali zao na askari wa Kenya.

Akijibu swali hilo, Dk. Angeline alibainisha kuwa kati ya alama hizo, 162 zilijengwa na kukarabatiwa na alama za kati 973 zilijengwa kwa umbali wa kati ya mita 100 na 200 ili kuwezesha wananchi kuubaini mpaka kwa urahisi.

Alisema uimarishwaji wa mpaka kati ya Ziwa Natron na Namanga wenye urefu wa Km 128 kwa mwaka 2019/20 uliahirishwa kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa Covid-19.

"Kutokana na uwapo wa ugonjwa huu, zoezi la kuimarisha mpaka uliobaki kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa Km 586 (nchi kavu) na Km 59.71 (ndani ya maji) limesimama hadi hapo nchi hizi mbili zitakapokubaliana," alisema.

Alifafanua kuwa urefu wa mpaka katika Wilaya ya Mkinga katika mpaka huo ambao haujaimarishwa ni Km 52.96 (nchi kavu).

Alisema sehemu ya mpaka ndani ya Bahari ya Hindi kutoka Jasini hadi kwenye alama ya utatu kati ya nchi za Tanzania, Kenya na Ushelisheli ina mkataba wa makubaliano kati ya Tanzania na Kenya ambao ulitiwa saini Juni 23, 2009 jijini Dar es Salaam lakini alama za mpaka (maboya) hazijawekwa.

Hata hivyo, alisema kazi ya kuweka maboya katika mpaka huo itafanyika baada ya kukamilika uimarishaji wa mpaka sehemu ya nchi kavu.

Alisema kuwa mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya una jumla ya urefu wa Km 817.71 (km. 758 nchi kavu na km. 59.71 ndani ya maji). Eneo la nchi kavu la mpaka huo linaanzia Ziwa Victoria, Wilaya ya Rorya mkoani Mara hadi Jasini, Wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga.

## Vijiji vyote kupata umeme mwakani

SERIKALI imesema mradi wa upelekaji umeme katika vijiji unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba mwakani.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza (CCM).

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini serikali utafikisha umeme kwenye vijiji visivyokuwa na nishati hiyo.

"Ni lini umeme utapelekwa katika Vijiji vya Buzi, Buguruka, Musina, Nsheshe na vingine ambavyo havijafikiwa na umeme katika Jimbo la Bukoba Vijijini?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea kupeleka umeme na kufikisha katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo Desemba 2022.

Alisema vijiji vinane kati ya 94 vya Bukoba Vijijini ambavyo ni Buzi, Buguruka, Musira, Nsheshe, Ngarama, Omubweya, Kagarama na Rukoma vinatarajiwa kupatiwa umeme kupitia REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili.


Alisema mradi huo huo ulianza kutekelezwa Machi mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Desemba mwakani kwa gharama Sh. bilioni 2.04.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA


Ukurasa 12

Manyara ina mtandao mdogo barabara, ila ubora wa ujenzi wake vinara kitaifa



Ukurasa 13

Chondechonde wabunge wetu Yarabi!


Ukurasa 14

**Sinema wachimba madini 'waliovamia' mashamba ekari 60, sasa mgodi dhahabu**



# Simulzi tata ya soko la Kimara Temboni lililotekwa na msuguano

**Na Yasmine Protace**

• Vilio uongozi, kodi, madai ya rushwa...



Biashara zikiendelea Kimara, pembezoni mwa Barabara ya Morogoro Kimara jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA eneo kando ya Barabara kuu ya Morogoro, kuna Soko Oliver Bitesigile la Temboni, ambalo ni maarufu jijini Dar es Salaam.

Ni soko maarufu lililoko katika Kata ya Saranga Mtaa wa Upendo, ndani ya wilaya na Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Umaarufu huo unatingwa na utata wa ndani yake, ikihusu makusanyo ya kodi za usafi, uongozi na hatima ya kuwapo kwake, kutokana na kukingana na barabara ya Morogoro.

Mbali na hilo, msuguano sawa ndani baina yao, tayari umeshawafikisha katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Hadi sasa, ukweli wa wajihi wake si soko rasmi, ingawaje matendo na huduma zake zinaufikia umma mkubwa.

Hata hivyo, ikiwa jumuiya rasmi ya kibishashara inayomtupa lawama rasmi, aliyekuwa Mwenyekiti wa Soko kwa miaka sita, Oliver Bitesigile, kwamba alikusanya pesa ya kuzoa taka na hesabu zake hazijulikani.

Pia, mahali hapo hapana huduma ya choo, hata wanalazimika kwenda kujisaidia katika vyoo jirani na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) walishawazuia kufanya ujezi wowote, kwa sababu ni eneo lililoko katika kingo za barabara.

Hata hivyo, hivi sasa wana uongozi mpya ambao Nipashe ulizungumza na Katibu wa Soko, Kudra Hussein, anayejigamba kwamba, watajiongoza kwa kufuata sheria ikiwamo na kufungua akaunti ya soko.

Anasema soko lina zaidi ya wafanyabiashara 100 na wanaolipa pesa ya usafi kwa kila mmoja, Sh. 500.

Anaahidi watahakikisha kuwa na uwazi katika ukusanyaji ushuru wa taka na malipo ya kusafisha soko. Gift Mwasimba, ni Mjumbe wa Wafanyabiashara Wadogo, anayesema mkakati walionao ni kuhakikisha taka zinazolewa kwa wakati, pia watafanya vikao na wafanyabiashara waelewe kinachokusanywa na kinachotoka.

Mageuzi hayo, ni tukio lilioendana na wafanyabiashara kufanya sherehe kumfurahia Mwenyekiti Oliver Bitesigile, kumaliza muda wake

### ANAYETUPIWA LAWAMA?

Nipashe ilipotaka ufafanuzi wa Mwenyekiti wa Soko aliyemaliza muda, Oliver, alijitetea kwamba, alishatumikia vipindi jumla miaka sita na kila wakati alielemewa na lawama, hata aliopotaka kujiuzulu, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, alimsihi asijiuzulu.

Anakana lawama dhidi yake, akianza na kutaja soko lina wafanyabiashara 160, lakini walipa kodi za taka ni 30 pekee, hata baadhi wakiombwa wanajibu wameshatoa kwa mgambo.

"Pesa nikusanye mimi, kwanini mgambo alipwe, halafu mnasema nachukuwa pesa, hamuoni ninachokifanya?" anahoji, huku akifahamisha mfanyausafi analipwa Sh. 10,000 kwa siku.

Pia, anasema gari la kuzoa taka linafika mara moja kila wiki, awali ilikuwa inalipwa Sh. 40,000 ikapanda hadi Sh. 80,000.

Kuhusu kukosekana choo, anasema alishachukua hatua, lakini akakutana na zuio kwamba sio soko la kudumu.

Pia, anasema alishakodi malori ya kukusanya taka, lakini ikawa hailipwi, kwa sababu ya wafanyabiashara kukataa kuchanga, wakaachana nayo, hata ilifika hatua anatoa pesa yake.

Anasema, wafanyabiashara wa soko hilo waliishamshitaki TAKUKURU, lakini hakukutwa na tuhuma akaachiwa huru, huku lawama zingine zikifika kwa Diwani wa Kata ya Saranga .

### SERIKALI MTAA

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Upendo, Gwelino Kalinga, anakiri soko lililoko katika hifadhi ya barabara, wafanyabiashara hawatakiwi kujenga mabanda ya kudumu.

Anasema, kazi iliyofanywa na serikali ya mtaa ni kusimamia soko na wakawataka wafanyabiashara wajichague wenyewe kuliendesha soko, kwa kufuata taratibu.

" Walijichagua wenyewe na ndipo walipoanza kuchangishana shilingi 500 ili zitumike kufanyia usafi wa soko," anasema.

Anakiri, pamoja na kukubaliana kuchanga,wapo wanaochanga na wapo wasiochanga na wamekuwa wakionywa wasiochanga.

Akizungumzia lawama za mwenyekiti aliyemaliza muda wake kukaa miaka sita, Kalinga anasema alichagukiwa kwa awamu na wafanyabiashara waliotokeza kugombea nafasi mbalimbali, ilipofikia penye uchaguzi walijitoa, wakimuachamwenyekiti huyo aliyemaliza muda wake.

Anakana tuhuma za makusanyo ya taka sio za kweli, kwani aliishajaribu kuwaunganisha wenye malori kusaidiana na mwenyekiti aliyemaliza muda wake, lakini nao walijitoa.

"Huyu mama (mwenyekiti wa zamani) alifanya kazi katika mazingira magumu hata ilifikia hatua mimi kutoa pesa yangu ili iweze kutumika kuzoa taka na kumpatia msafisha soko," anasema.

Anasema taarifa za soko zimekuwa zikisomwa kila baada ya miezi mitatu na msuguano kati yao na mwenyekiti wa aliyeondoka, alipinga biashara kufanyika katika hifadhi ya barabara wakati ujenzi unaendelea.

UCHUMI

NAIBU WAZIRI UJENZI:

# Manyara ina mtandao mdogo barabara, ila ubora wa ujenzi wake vinara kitaifa

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

- Daraja 'pasua kichwa' miaka nenda rudi rasmi
- Yashangiliwa uchumi juu hadi Tanga, Dodoma

MANYARA ni mkoa unaotajwa kuwa kuwa mtandao mdogo wa barabara, lakini unatajwa na serikali kuwa imejengwa katika ubora uliotukuka kitaifa.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, katika ziara yake mkoani hapa analiibua hilo anapozungumza na wafanyakazi wa taasisi zilizo chini ya wizara yake, ikiwamo Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Mhandisi Kasekenya anafafanua:"Manyara ina 'network' (mtandao ) ndogo sana ya barabara ndio maana serikali inataka kuongeza mtandao wa barabara,"

Naibu Waziri anasema aliamua kufanya ziara mkoani humo kuziona barabara za mkoa, ili apate namna ya kuzitetea kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, akifafanua kwamba alishakutana na wanasiasa wa mkoa huo na waliomueleza kuridhishwa na utendaji wa TANROADS kimkoa.

"Wanasema barabara za Manyara ni bora zaidi kuliko za mikoa yote Tanzanian," anafafanua na kuongeza: "Si mnaona wabunge wengi 'wana- fight' (wanapigana) wakiomba barabara zao zipandishwe hadhi ili ziende TANROADS kwa kuwa zitasimamiwa vizuri."

Kiongozi huyo anasisitiza haja ya umakini wa makandarasi, viginevyo wanakaribisha 'kutumbuliwa' inayoishia hatari kampuni zao kufilisika

"Hatutegemei mtu professional (mtaaluma) afanye mambo ya ajabu, bali tunatakiwa kuheshimiana na kama kuna mtu atafanya tofauti hakuna mtu atamlinda. Kazi tunataka zifanyike, ila tuangalie 'value for money' (thamani ya pesa) kama ipo kwenye barabara, maana serikali inaziangalia...kwa taasisi zote," anasema Naibu Waziri Kasekenya

### DARAJA MAGARA

Katika Daraja la Magara wilayani Babati, aliridhishwa na ujenzi wake, akisema ni miradi michache inayokamilika ndani ya muda uliopangwa na akawapongeza TANROADS kwa mafanikio hayo.

Anasema, kumekuwapo tatizo la mifugo kuharibu barabara, hivyo ni muhimu kuwategenezea njia rasilimali hiyo akiwakumbusha wananchi:"Daraja hili si la serikali bali la wananchi, hivyo wana wajibu kulilinda na kuheshimu alama za barabarani."

Pia, anawataka wananchi wasilime kwenye Hifadhi ya Barabara, ili kusaidia kulinda barabara akisema anafurahi Kijiji cha Magara kimeingia mkataba na TANROADS kulinda daraja hilo.

Katika kata ya Hydom, wilayani Mbulu, anawahakikishia wakazi ahadi za Hayati Rais Dk. John Magufuli na yaliyoahidiwa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) zitatekelezwa.

Naibu Waziri Kasekenya, anasema muda wowote wataanza kujenga barabara kati ya Hydom/Mbulu hadi Maswa kwa kiwango cha lami kabla kwisha kwa mwaka uliopo wa fedha.

Kasekenya ambaye pia ni Mbunge wa Ileje, anasema ndani ya muda mfupi ujao kutatangazwa kuanza ujenzi wake, kukiwapo matarajio utakuzwa uchumi wa nchi na mataifa jirani.

Katika ziara hiyo, alikagua barabara za Bassout wilayani Hanan'g na nyingine za Gallapo, Chubi hadi Kutish itakayojengwa hadi wilaya ya Kiteto na kunaelezwa matarajio ya kufungua uchumi wa mkoa huo na majirani kama Tanga na Dodoma.



Naibu waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wa nne kutoka kulia), akiteta jambo na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, (wa pili kutoka Kulia) alipokagua Daraja la Magara mkoani Manyara. **PICHA ZOTE: JALIWASON JASSON**

> **Muda wowote wataanza kujenga barabara kati ya Hydom/Mbulu hadi Maswa kwa kiwango cha lami kabla kwisha kwa mwaka uliopo wa fedha.**



Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Manyara, Mhandisi Bashir Rwesingisa (wa kwanza kulia), akimwonyesha Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wa tatu kutoka kulia), linavyojengwa 'daraja korofi' la Chubi kwenda Kutish.

### KUTOKA TANROADS

Meneja wa TANROADS Manyara, Mhandisi Bashir Rwesingisa, anasema kuwa katika mkoa huo wanazihudumia barabara kilometa 1656.

Anazumgumzia mradi mkubwa wa kujenda Daraja la Magara, lililopo umbali kilometa 21 kutoka barabara kuu iendayo Arusha eneo la Mbuyu wa Mjerumani, ulikamilika na kukabidhiwa kwa serikali Febuari 14 mwaka uliopita.

Mhandisi Rwesingisa, anasema kipindi cha matazamio cha mwaka mmoja kimeisha Februari 13, mwaka huu na sasa umezinduliwa rasmi mwezi huu, ikiunganisha Wilaya za Babati na Mbulu, akiwa anashuhudia: "Mpaka sasa hatujaona tatizo lolote kutokana na ujenzi hafifu,"

Kwa mujibu wa Mhandisi Rwesingisa, ujenzi wa darala la Magara, ulitekelezwa na Mkadarasi China Railway Group kwa gharama Sh. bilioni 12.641 kwa muda wa miezi 24, kazi iliyoanza rasmi Februari 2018.

Anachanganua maudhui ya mradi ni kujenga daraja lenye urefu wa mita 84, likiwa na sehemu tatu zenye mita 24 sehemu mbili pembeni kila moja ina mita 36. Mhandisi Rwesingisa anataja lingine ni kujengwa daraja dogo lenye makeravati 18 na taa za barabarani daraja, kuimarisha usalama wake.

Pia, kuna barabara unganishi ya kilomita 5.2, kati yake barabara kilometa 3.8 za kiwango cha lami na kilometa 1.4 zimejengwa kiwango cha changarawe.

Anavitaja vikwazo vinavyowakumba wakati wanajenga barabara kuwa ni uhaba wa kokoto kwa makandarasi walilazimika kuzisafirisha kutoka Mwanza na Bukoba, kuongezeka kwa maji Ziwa Bassoutu na uhaba wa maji wilayani Simanjiro na Kiteto.

Meneja wa TANROADS anakiri ukosefu wa makandarasi wenye uwezo kwa kazi za madaraja, imechangia makandarasi wengi wanakimbia miradi.

### MAJIRANI HIFADHINI

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara, Noelia Myonga, anasema ujenzi wa daraja hilo una manufaa kwa wagemi wa hifadhi kwa kurahisisha mawasiliano ya usafiri wa watalii watokao Hifadhi ya Taifa Tarangire hadi Manyara, wanaotumia nusdi saa pekee kuwafikia.

Myonga anasemaa katika kasoro ya zamani, wasafiri hao wengi wa kitalii, walilazimika kuzungukia eneo la Mto wa Mbu walikotumia muda wa saa moja na nusu kufika hifadhini, huku kukiwapo historia watalii walipofika Mto Magara na kukuta umefurika maji, walirejea walikotoka.

### WANANCHI WASEMAJE?

Diwani Mstaafu wa Kata ya Magara, John Dim, anaipongeza TANROADS na anakiri kuwa baada ya ujenzi wa daraja hilo, wanashuhdia manufaa, ikiwamo kwa wanafunzi waliokuwa wanakwama njiani ,mtyo unaopofurika.


Dim anasema wanafunzi waliata shida na kuna wakati walitumia saa kadhaa kusubiri uwezakano vwa maji kupungua na anadai magari kutoka wilaya ya Mbulu yalikuwa yanakatiza safari zake, hata kwa siku kadhaa amji yanayopokuwa mengi.

Leonard Emmanuel, mkazi wa Kijiji cha Magara, anatoa uzoefu wa watoto wake, kwamba walikwama kwenda shule na yeye akashindwa kwenda shambani kwake. Emmanuel amekuwa akilazimika kuwavusha watoto wake waende shule, jukumu lililomgharimu saa nane hadi tano na walipofika shule, walikuwa wanasoma somo moja tu na mengine walikuwa yameshawapita.

Mkazi huyo anaelekeza shukrani kwa Rais wa kipindi kilichopita, Hayati Dk. John Magufuli, kwamba ndioyer aliifanyia na kufikia hatua mafanikio hayo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Chondechonde wabunge wetu Yarabi!






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

WAKATI naripoti habari za Bunge enzi hizo, siku moja nikiwa nimejaliwa katika chumba wanamokaa waandishi wa habari bungeni, tukisubiri kuanza kwa kipindi cha maswali na majibu, ghafla alinifuata msimamizi wetu, akitokea Idara ya Habari MAELEZO, namkumbuka kwa jina moja la Ponela.

Nikiwa katika suti yangu ya mtumba rangi ya kijani kibichi, ikiwa ni mara ya kwanza kuivaa bungeni, akanisogelea na kuninong'oneza kiungwana kabisa, "aisee kabadili suti haifai hapa bungeni hiyo." Nikajishitukia na kweli nilipoangalia haikuwa inafaa. Nilivalia koti lisilo na ukosi na ndani sikuwa na shati, kwa sababu halikuhitajika, lakini kumbe haikustahili kwa kuwa aina ya suti zilizokuwa zinakubaliwa, ni zilizoruhusu shati ndani na tai juu yake. Sikuwa na tai wala shati ndani.

Kwa heshima kabisa, nikatoka nje na kuchukua teksi kurudi nyumba ya kulala wageni niliyofikia. Kumbuka enzi hizo hakukuwa na bodaboda, ila zilikuwapo pikipiki, lakini si za biashara. Hivyo, nisingeweza kukodi, hazikuruhusiwa, bajaji ndo usiseme, hazikuwapo kabisaa!

Huyoo na teksi mpaka 'gesti', nikamwomba dereva teksi anisubiri kwa malipo ya ziada, nikaingia ndani nikabadili na kuvaa suti mwafaka na kurejea bungeni, nikakuta maswali na majibu yakiendelea. Nikajifunza, kuwa kumbe kila kitu au mahali na nidhamu yake.

Bungeni ni mahali ambako nidhamu inazingatiwa sana, nadhani kuliko mahali kwingine, ambako nilipata kufika na kupajua. Bungeni ni mwendo wa suti na kwa wanawake kama si suti, basi vazi la heshima, si 'vimini' au nguo zisizo na staha. Ukikiuka tu, kuna askari mle hawachelewi kukufurumua.

Mtu kuwa mbunge ni heshima kubwa katika jamii. Ni mwakilishi wa jamii na anachaguliwa na jamii, hivyo ni kioo cha jamii husika. Anavyojiheshimu, ndivyo pia jamii inavyomheshimu, hivyo anatakiwa kutunza hadhi na heshima yake, ili iendane pia na jamii anayoiwakilisha.

Ubunge ni hatua ya kufikia uwaziri na hata urais ikiwezekana. Ushahidi ni nchini ambako marais sita mpaka sasa, wana historia ya kuwa wabunge. Hivyo, ni jambo la kuangalia na kulienzi sana. Ni nafasi adhimu katika jamii.

Hivi karibuni, nikamsikia Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiwasihi wabunge dhidi ya kupanda bodaboda kwenda na kurudi bungeni. Mpaka afungue kinywa kuyasema hayo, ina maana yalishamgusa na kuona kwa vyovyote haistahili.

Akawaambia, pamoja na kwamba ni usafiri nafuu na wa haraka, lakini ni hatari na hasa ikizingatiwa, kuwa ubunge ni gharama. Kwa kweli haiji, kwa mbunge, mwakilishi wa jimbo, mwenye kura za wananchi maelfu, kupanda bodaboda kwenda bungeni!

Unafika bungeni unafuta machozi, kutokana na upepo wa bodaboda huko njiani! Hebu fikiria mbali na huo upepo, bodaboda mara imepata ajali mbunge umevunjika mguu! Kisa unafuu na haraka? Jamani tuangalie na hadhi zetu basi, kama hatutaki basi za majimbo yetu je?

Mbunge achilia mbali mshahara, una posho ya kikao ambayo si haba, una mkopo wa gari na unalo, ya nini kuparamia bodaboda Yarabi? Yakukute ya kukukuta, uvunjike mguu, ulazwe hospitalini na maantena mguuni, nani atawakilisha wananchi wako?

Serikali ilizingatia umuhimu wa mbunge na ndiyo sababu ikaweka fursa ya mbunge kuwa na usafiri wa uhakika, wa kumpeleka maeneo mbalimbali jimboni mwake, pia kumpeleka bungeni na kurudi, sasa iweje fursa hiyo iwekwe pembeni mbunge udandie bodaboda? Basi kama lazima panda bajaji, angalau hiyo bodi si mwili wako!

Nadhani ifike mahali kuwepo na sheria ndogo, itakayozuia waheshimiwa hawa kupanda bodaboda, ili kulinda uheshimiwa wao na uheshimiwa wa majimbo yao, kuhakikisha wako salama muda wote wanapokuwa wawakilishi wa wananchi.

Yawezekana kuna baadhi yao hawajui umuhimu wao kwa jamii, bunge na serikali. Labda pengine, wapo wanaojiona bado ni vijana sana, hata kupanda bodaboda. Lakini wakumbuke, ndiyo sababu kama hujafikia umri wa kuoa au kuolewa, wazee hawakuruhusu ufanye hivyo. Jitambueni basi. Alamsiki!

BIASHARA

MAMBO YA MBOGWE – GEITA

# Sinema wachimba madini 'waliovamia' shamba ekari 60, sasa mgodi dhahabu

• Walivamia na magari, wakafikia gesti kisha wakaanza kuchimba • Usimamizi wake ni wa kienyeji: RC, DC na Ofisa Madini wanasema ripoti yenye ukweli inakuja

**Na Richard Makore,** aliyekuwa MBOGWE



Wachimbaji wa Nyakafuru, Mbogwe, walipomsikiliza Naibu Waziri wa Madini, Nyongo (picha ndogo). **PICHA: MTANDAO**

NI umbali wa zaidi ya kilomita 120 kutoka Geita mjini, katika kijiji kinachoitwa Nyakafuru. Hali haikuwa nzuri mahali hapo, wakulima na wachimba madini wako katika msuguano kugombea ardhi.

Mara baada ya Nipashe 'kutia timu' siku chache zilizopita na kisha kuweka kambi mahali hapo, ushuhuda wake wa kwanza ilikutana na zaidi ya wakazi 200 wanaojitambulisha kutoka kaya 22, 'wamiliki wa mashamba' kijijini Nyakafuru, Wilayani Mbogwe.

Wanajieleza kuwa wadau na wenyeji wa shughuli zilizo bayana za kilimo, ufugaji na biashara ndogo zinazofanyika kando ya barabara ya Kahama kuelekea mikoa ya Kagera, Kigoma na nchi jirani za Rwanda na Burundi, hata kuimarisha uchumi wa mahali hapo, bila kusahau nyumba za kulala wageni. .

Hata hivyo, uhusiano baina ya pande hizo mbili si njema hata kidogo, wakulima wamewanunia wachimba madini wadogo wakionekana 'waonevu.'

Ni kijiji chenye idadi kubwa ya watu kutokana na shughuli zinazofanyika hapo, huku wanaoitwa 'wavamizi' wenyewe wakiwa na zaidi ya miaka mitatu sasa wanajinasibu kwa siku mgodi huo unatoa wastani wa kilo moja ya dhahabu kwa siku, yenye thamani zaidi ya Sh. Milioni 100.

### MKASA ULIKUWAJE?

Katibu wa wananchi hao walioporwa mashamba, Shariff Omary, anaiambia Nipashe kuwa uvamizi huo wa wachimbaji wadogo, ulikuwa katika namna ya kupangwa, kukiwapo kundi la watu waliofika kwenye magari maalum ya kukodi lilingia kijijini hapo.

Anasema baada tu ya kufika, walianza kununua zana za kuchimba dhahabu kama vile sululu, koleo, moko, karai, kamba na kwamba wenyeji wa kijiji hicho wanasema siku hiyo nyumba zote za kulala wageni zilifurika na vyakula vyote viliisha kwenye migahawa.

Omary anasema, ulikuwa uvamizi anaoufananisha kama wa kijeshi, kwa sababu wakulima hawakupata nafasi za kujitetea kuhusu mashamba yao na kwa takribani siku mbili Nipashe ilipokuwa kijijini hapo, ilibaibini wachimbaji hao wote wanatoka nje ya kijiji na vijana wazawa wanabaki mashuhuda wa kinachoendelea kwao.

> **"Baada ya uvamizi huo imesimamisha kazi hiyo na iwapo suala hilo litafika tamati na watafiti hao wakitaka kuendeleza na shughuli zao, watapatiwa leseni watapewa.**

Hata hivyo, baadhi yao wanaweka bayana kwamba fedha nyingi 'wanazovuna' kutoka kwenye madini, zinachukuliwa na matajiri wachache waliojificha nyuma ya wachimbaji hao, kwa kuwa hakuna udhibiti wa serikali katika 'mgodi mpori' huo.

Omary anasema, katika miaka ya nyuma kabla mashamba yao kuanza kufanyiwa utafiti wa madini na kampuni ya Mabangu, walikuwa wanalima mazao mbalimbali, yakiwamo mahindi na pamba na sasa wamelazimika kuyaacha kabla kikundi hicho maarufu 'Isanjabadugu; kuingia kwakivuli cha wachimbaji wadogo mwaka 2017.

Anasema, eneo waliloporwa ni jumla ya mashamba 30 yenye ukubwa wa ekari 60 na kwa sasa kikundi hicho kinafanya uchimbaji dhahabu kwa ufadhili wa wanaitwa 'matajiri.'

Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Juma Mageta, alipotakiwa kuifafanua mkasa, anakiri vijana hao wanaojiita Isanjabadugu, wanachimba dhahabu usiku na mchana na



kuendelea kuharibu mashamba waliyoyakuta ya wakulima, huku akidai kijiji hakinufaiki.

### OFISA MADINI

Dodosa za Nipashe kijijini haikuweza kumpata mchimba madini aliyekuwa tayari kuongea kwa uwazi, ingawaje ilibaini utaratibu wa Ofisi ya Madini, inasubiri kupewa taarifa kutoka kwa wamiliki wa mashimo hayo, pasipo kufuatilia kwa karibu uhalisia wa kinachopatikana, ili serikali kupata mrahaba na kodi sahihi.

Sera ya Madini nchini, intafsiri kwamba wachimbaji wadogo wanatakiwa kutumia eneo lisilozidi hekta 10. Hivi sasa wakazi hao wa Nyakafuru, wanamtaka Rais Samia Hassan kuwasaidia kuwaondoa wachimba madini hao kikundi cha Isanjabadugu.

Katibu wa wananchi hao, Omary, anasema waliwahi kutoa kilio chao kwa Hayati Rais John Magufuli, aliyeagiza suala hilo lipatiwe ufumbuzi, lakini hadi sasa wameshindwa kupata haki yao.

Wananchi hao ambao walikuwa wanatumia mashamba hayo kwa ajili ya shughuli za kilimo, walifukuzwa katika maeneo hayo na kikundi hicho kinachodaiwa kufadhiliwa na mtandao wa watu wenye uwezo kifedha mkoani Geita.

### SERIKALI GEITA

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Madini Mkazi mkoani Geita, Daniel Mapunda, anakiri kuwapo mgogoro huo na kwamba unashughulikiwa kwa ngazi ya mkoa.

Mapunda anasema, anatambua wananchi hao wenye mashamba na kwamba suala hilo liliundiwa kamati na mkoa ambayo iliendа kufanya uchunguzi kujua ukweli na majibu yatatolewa na Mkuu wa Mkoa Robert Gabriel.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha John, anakiri kuwapo wavamizi hao na kwamba serikali inafanya utaratibu kubaini wenye mashamba halali, ili haki ipatikane katika mustakabali sahihi. Anakiri kikundi cha Isanjabadugu kuchimba dhahabu bila kibali, ikiwamo leseni ya uchmbaji, ingawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, inaendelea kukusanya mapato, kutokana na uchimbaji huo.

Mkuu wa Wilaya, anakumbusha historia kwamba walivamia eneo hilo na kuanza shughuli za uchimbaji tangu mwaka 2017 na hadi sasa Kamati ya Mkuu wa Mkoa, ndio ina mamlaka ya kutoa majibu, baada ya kumaliza uchunguzi wake.

Mkuu huyo wa Wilaya, anasema, mashamba hayo kabla ya kuvamiwa yalikuwa yakifanyiwa utafiti kubaini kama kuna dhahabu na kampuni ya Mabangu, iliyokuwa na leseni halali kwa ajili ya utafiti huo wa madini.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, anazungumzia mkasa huo kwamba, kamati aliyounda imeshamaliza kazi yake na kwamba ripoti itapelekwa katika Wizara ya Madini.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, ni kamati iliyohusisha watalaamu wa masuala ya madini, ardhi, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na maofisa wengine wa serikali na kwamba muda wote ataitoa ripoti hiyo.

Anasema aliiunda kwa agizo la Hayati Rais Dk. Magufuli na kwamba katika uchunguzi wao waliangalia vielelezo mbalimbali kuhusu umiliki wa ardhi katika eneo hilo.



## HABARI DODOMA




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara (wa pili kushoto), akisisitiza jambo kwa Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Heriel Mteri (kulia), wakati akikagua moja ya vifaa vya kisasa vya matengenezo ya magari ya Serikali vilivyopo katika karakana ya wakala huo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: TEMESA**

# Mpango wa TASAF wapunguza umaskini wa kaya kwa asilimia 12

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MPANGO wa kunusuru kaya maskini unotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umechangia kufikiwa kwa azma ya serikali ya kupunguza umaskini.

Takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa kaya umepungua kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya maskini nchini.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezalia Makota, alipokuwa akifungua kikao kazi cha kujengewa uelewa wadau kuhusu sehemu ya pili ya TASAF awamu ya tatu.

Pia alisema utekelezaji wa mpango huo umewezesha kaya za walengwa kujikita kwenye shughuli za kukuza kipato na kujiimarisha kiuchumi ikiwamo ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara ndogo ndogo.

"Pamoja na mafanikio hayo, vijiji, mitaa, shehia zilizofikiwa katika kipindi cha kwanza ni asilimia 70, hivyo bado kuna wananchi wanaoishi katika hali duni kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa," alisema.

Makota alisema baada ya kukamilika kwa kipindi cha kwanza serikali iliamua kuendelea na kipindi cha pili katika awamu ya tatu ya TASAF ili kaya zote zinazoishi katika mazingira duni, zipate usaidizi.

"Tofauti na sehemu ya kwanza, kipindi cha pili cha awamu ya tatu (TASAF III) kitatekelezwa katika halmashauri zote 184 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar," alisema

Alisema kuwa utekelezaji huo utafanyika kwenye vijiji, mitaa, shehia zote nchini na kujumuisha maeneo yote ambayo hayakupata fursa hiyo katika kipindi cha kwanza.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wadau wote watakao husika katika mpango huo katika kipindi hichi cha pili cha TASAF awamu ya tatu kuzingatia utaratibu uliwekwa na serikali.

"Sitapenda kusikia katika wilaya yangu kuna kaya ambayo haina sifa imeingizwa kwenye mpango huu. Kasimamieni maelezo na kiapo ambacho mmeapa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Awali, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Japhet Boaz, akizungumza katika kikao hicho, alisema kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kitazifikia kaya 1,450,000 zenye takribani zaidi ya watu milioni saba nchini kote ikiwa ni nyongeza ya kaya 300,000.

# Wataka sheria uanzishaji kampuni za ulinzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Sekta ya Ulinzi Binafsi Tanzania (TSIA) kimeiomba serikali kuruhusiwa kutunga sheria itakayotumika kuongoza kampuni zao.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Wamiliki wa Kampuni za Ulinzia Binafsi nchini, Felix Kagisa, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa kanda ya kati uliofanyika jijini hapa.

Alisema kampuni za ulinzi ya sekta binafsi zimeonekana kutokufanya vizuri kutokana na kutokuwa na sheria yao hali inayosababisha kuanzishwa kwa kampuni nyingi zisizo na sifa wala vigezo.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vyema sasa serikali ikawaruhusu kuwa na sheria hiyo ili kudhibiti uanzishwaji holela wa kampuni ambazo zimekuwa zikianzishwa bila kufuta utaratibu na kanuni zake.

"Kumekuwapo na utitiri wa kampuni binafsi za ulinzi ambazo hazizingatii sheria, hali ambayo inasababisha hata kwenye ajira ya kuajiri walinzi, hazifuati kanuni na vigezo," alisema.

Aidha, chama hicho kimeiomba serikali kuona namna ya kubadili sheria ya umiliki wa silaha kwa kuwa iliyopo ni kandamizi kwao na hairahisishi upatikanaji wa silaha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yako.

Awali, akizungumza baada ya kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, alizitaka kampuni za ulinzi binafsi kuzingati miongozo inayotolewa na jeshi la polisi na kufanya kazi kulingana na vibali vyao.

Pia alizishauri kampuni hizo kutokuajiri watu wenyewe umri zaidi ya miaka 45 kwenye kazi za ulinzi kwa umri huo hauendani na shughuli za kiulinzi, badala yake waajiri kama wajumbe au washauri.

Alisema pamoja na vigezo na sifa walizo nazo wazee hao, kwa umri walio nao kwenye utendaji wao hautakuwa kama ilivyo kwa wenye miaka chini ya 45.

Katika uchaguzi huo chama hicho kiliwachagua mbali na Kayombo, makamu wake ni Mathias Matimbwi, Katibu ni John Zacharia, katibu msaidizi Emmanuel Kapaya na mtunza hazina Fidelis Luhunga.

# Waislam wapewa somo Ramadhani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEIKH wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewataka waumini wa dini ya Kiislamu kuutumia mwezi mtukufu wa Ramadhani kufanya matendo mema katika jamii pamoja na kutunza amani iliyopo kwa kipindi chote cha mfungo.

Sheikh Rajabu alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfugo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Alisema katika mwezi wa Ramadhani, waumini hawapaswi kutenda maovu, bali wautumie muda huu kufanya dua, kusaidia wenye uhitaji katika maeneo yao ili kudumisha umoja na mshikamano.

Pia alisema mwezi huu ni vyema watu wakafanya mema huku wakitambua kuwa kuna waumini wengine wana matatizo mengi mitaani, hivyo wanatakiwa kuguswa na kuwasaidia.

"Tuutumie mwezi huu kwa amani kwa sababu Mtume Muhammad mwenyewe anasema kwamba nimekuja mimi kwa ajili ya kutimiza tabia njema, tabia tukufu na anasema ametimilizwa kwa kuwa yeye ni mwalimu wa kuelimisha watu mambo yaliyokuwa mema, mazuri watu wayafanye na kuonya watu waache matendo maovu yanayoweza kuwasababishia kuuingia moto wa Mungu," alisema.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu kufanya maasi inapokaribia kipindi cha mfungo kwa madai ya kujiandaa na mfungo bila kujua kufanya hivyo ni dhambi.

"Kuna kitu kimezuka kinaitwa vunja jungu yaani wakikusudia kufanya maasi ya mwisho eti kwa ajili ya mwezi mtukufu. Hawaelewi kwamba hata huu mwezi wanaouaga nao ni mwezi mtukufu maana ni miezi mitukufu mitatu imefuatana kuna mwezi wa Rajabu ambao umeuachia Shaban na Shaban umeuachia Ramadhan.

"Kwa hiyo mwezi wa Rajabu ni kama vile shamba linaloandaliwa na mtu kwa kutiliwa mbolea, Shaban ni mwezi wa kupanda na kupalilia na Ramadhan ni mwezi wa mavuno," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza kuu la Bakwata Wilaya, Bashiru Omary aliwataka waumini wa dini ya kiislamu wanaofunga kuwa na hofu ya Mungu pamoja na kufanya ukarimu kwa wengine.

Alisema kinachotakiwa ni kuzingatia funga yao wafanye yanayotakiwa katika mfungo huo na kufanya ibada zaidi.





# RC aonyesha wasiwasi jiji kugawanywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LICHA ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Mbeya kupendekeza kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ya Uyole ambayo itatokana na kugawanywa kwa jiji hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema watahitaji nguvu kubwa kushawishi kutokana na eneo hilo kukosa baadhi ya sifa muhimu.

Chalamila alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa majengo mapya ya Hospitali ya Igawilo ambayo imepandishwa hadhi kutoka Kituo cha Afya na kuwa hospitali ya Wilaya.

Alisema maeneo mengi ya halmashauri hiyo hayajapimwa, hivyo makazi ya wananchi yamejengwa holela na hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za umma yakiwamo masoko.

"Hili bonde lote la Uyole limependekezwa iwe Halmashauri inayojitegemea lakini inaweza isiwe na sifa sana mpaka tutakapopiga magoti tujieleze vizuri. Maeneo mengi ni 'squatter' (makazi holela) na hakuna sehemu tunaweza kuonyesha soko zuri," alisema Chalamila.

Pia alisema eneo hilo halina barabara nzuri ambazo zinaweza kuifanya halmashauri hiyo mpya kuwa na sifa za kujitegemea, hivyo akadai kuwa kitakachofanyika ni kuupanga vizuri mji huo.

Alisema wameanza kuwalipa wananchi fidia ili nyumba zao zibomolewe, viwanja vipimwe na makazi yapimwe vizuri ili angalau mji huo upangike vizuri.

Sambamba na hayo, alisema wameanzia kupima eneo la Iduda ambalo vimepatikana viwanja 528 ambavyo vitaanza kuuzwa hivi karibuni na kwamba wananchi tayari wameshaanza kulipwa fidia.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema katika eneo hilo halmashauri ilitakiwa kuwalipa wananchi fidia ya Sh. bilioni 1.5 ili wapishe mchakato wa upimaji.

Alisema mpaka sasa wameshalipa Sh. bilioni 1.1 na zimebaki Sh. milioni 400 ambazo alisema mchakato wa kulipa unaendelea na kwamba ukikamilika watalipa.

Ng'wanidako alisema viwanja hivyo vitaanza kuuzwa wiki ijayo kwa gharama ya Sh. 8,500 kila mita moja ya mraba, hivyo akasisitiza kwamba wananchi wajitokeze kuvinunua.

"Vimeshakamilika na wiki ijayo tunatarajia kutoa tangazo la kuanza kuviuza rasmi. Vipo viwanja vya makazi, vya biashara na vya taasisi mbalimbali," alisema Ng'wanidako.

Naye Meya wa Jiji la Mbeya, Dur Issa Mohamed, alisema wanaendelea kushirikiana na watendaji wa halmashauri pamoja na wadau wengine kukamilisha miradi mbalimbali ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kuanza kuwanufaisha wananchi. Alisema wanafuatilia kila siku maendeleo ya ujenzi wa hospitali ya Igawilo ambayo wamepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha majengo yanayoendelea kujengwa.

Mchakato wa kuligawa Jiji la Mbeya ili kuzalisha halmashauri mpya ya Uyole unaendelea na mpaka sasa wanaendelea kukusanya maoni kabla ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC), Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na hatimaye wizarani.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki (wa pili kushoto), akikabidhi mashine ya kisasa ya kupigapiga maharage kwa Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima wa maharage cha Upendo cha Wilayani Mbozi, mkoani Songwe, Daud Bukuku, iliyotolewa na kituo hicho kwa ushirikiano na Taasisi ya kimataifa ya mazao ya kitropiki ya CIAT, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TADB yapania kuwaendeleza wakulima, wafugaji na wavuvi

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

UONGOZI wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) umesema unakusudia kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi wa Wilaya ya Kyela kuongeza tija kwa kuviongezea mtaji vyama vya msingi vya ushirika.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, aliyasema hayo juzi alipowaongoza wajumbe wa benki hiyo kutembelea wilaya hiyo kwa lengo la kuangalia fursa zilizoko na namna ya kuongeza tija kwenye shughuli hizo.

Alisema lengo lao ni kutaka kupata miradi mitatu itakayowawezesha vijana na wanawake ili benki hiyo iwasaidie kuboresha mnyororo wa thamani kwenye shughuli zao za uzalishaji.

"Tuko tayari kuwezesha mitaji kwa vyama vya msingi ili vinunuwe mazao ya wakulima na kulipa kwa wakati na wakulima wawe wananufaika kwa kuongeza uzalishaji na hata kufanya shughuli zingine za maendeleo," alisema Justine.

Alisema benki hiyo inalenga kuongeza tija katika zao la kakao ambalo lina thamani kubwa na uhitaji wake katika soko la dunia ni mkubwa na kwamba katika mwaka uliopita pamoja na tatizo la corona, wilaya kupitia vyama vya msingi 69, iliuza zaidi ya tani 10,000.

Alisema taarifa walizo nazo ni kwamba wakulima wa waliuza kakao hiyo kwa zaidi ya Sh. bilioni 50 na kwamba ni ishara nzuri kwa maendeleo ya zao hilo huku akidai kuwa watasaidia kuongeza zaidi mauzo.

Tanzania, alisema huchangia asilimia 0.2 pekee ya kakao duniani na kwamba kwa sasa kuna taarifa kuwa uzalishaji wa zao hilo nchini umeshuka.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta, alisema Kyela ina fursa kubwa katika kilimo cha kakao, zao ambalo karibu kila mwanachi amepanda miti ya zao hilo.

Alisema kwa sasa zao hilo linauzwa kwa njia ya mnada kupitia vyama vya ushirika lakini kuna matatizo ambayo yanaibuka kwenye soko la zao hilo ikiwamo madalali kuwanyonya wakulima kwa kununua mazao yao kwa bei ndogo.

Kitta alisema madalali hao ambao wanajulikana zaidi kwa jina la 'Njemke' huwa wanatumia mwanya wa ukosefu wa mitaji kwa wakulima na vyama vya ushirika kuingia mitaani na kununua mazao ya wakulima. "Hii inasababisha wakulima wengi kuuza kwa faida ndogo sana kwa madalali ambao wao huenda kuuza kwa faida mara mbili zaidi, hii inakatisha tamaa wakulima," alisema Kitta.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, aliuambia ujumbe wa benki hiyo kuwa azma ya halmshauri si kutonufaika na kilimo pekee bali pamoja na sekta zingine ikiwamo uvuvi kutokana na uwapo wa Ziwa Nyasa.

Pamoja na kuzungumza na uongozi wa wilaya, mkurugenzi mtendaji wa TADB alitembelea Chama cha Msingi cha Mababu CCF, kilichoko wilayani hapa ambacho hujishughulisha na kukausha kakao.

Halmashauri ya wilaya ya Kyela ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa zao la kakao katika Mkoa wa Mbeya ikifuatiwa na Rungwe na Busokelo.

# Wakulima wa soya wapata neema soko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa soya nchini wametangaziwa neema ya soko la uhakika ambalo limepatikana nchini China ambako zao hilo linahitajika kwa wingi.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema tayari Tanzania imeingia makubaliano na China kwa ajili ya kuuza soya nchini humo.

Bucheyeki alisema ili kukidhi soko hilo, taasisi yake imeanza uzalishaji wa mbegu za zao hilo kwa wingi ili kuzisambaza kwa wakulima ambao watazalisha kwa wingi.

"Sisi kama TARI tumeanza kuzalisha mbegu nyingi na za aina mbalimbali za soya kwa ajili ya kuwasambazia wakulima. Lakini pia tunalo jukumu lingine la kuhamasisha kilimo cha zao hili kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko ambalo serikali yetu imelipata nchini China," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema soko hilo linahitaji soya kwa wingi kuanzia sasa, hivyo ili kutolipoteza serikali imeamua hata kuruhusu wakulima kutoka nchi jirani kuuza soya yao nchini Tanzania ili isafirishwe kwenda China wakati Tanzania yenyewe ikiwajengea uwezo wakulima wake.

"Tunajua kwa sasa wakulima wetu hawezi kukidhi soko kubwa tulilolipata huko China, hivyo mbinu tunayoitumia ili tusilipoteze soko hili ni kwa sasa kupata soya hata kutoka nje hasa kwa nchi majirani," alisema Bucheyeki.

Alisema TARI imejiwekea mikakati ya kuhakikisha soya inazalishwa kwa wingi kuanzia mwakani na wakulima wa ndani ya nchi ambayo itanunuliwa kwa bei nzuri na kwenda kuuzwa China.

Mkurugenzi huyo alisema kupatikana kwa soko hilo la uhakika, TARI itahamasisha wakulima wengi kulima zao hilo kwa vile kuna uhakika wa wakulima wa zao hilo kunafaika mara dufu kupitia soko hilo.





# Wanachama SACCOS, Vikoba Zanzibar wapewa matumaini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, imesema kukamilika kwa sheria ya huduma ndogo za kifedha itasaidia kuweka usalama wa fedha za wananchi kupitia benki, vikundi vya kuweka na kukopa.(SACCOS)

Mwenyekiti wa tume hiyo, Khadija Shamte, Mzee, aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao kilichoshirikisha tasisi za umma zinazohusika na sheria ndogo za kifedha. Aidha, alisema sheria hiyo inalenga kuweka utaratibu mzuri wa fedha za wateja na zinakuwa salama kwa kuzisimamia ipasavyo.

Alisema kabla ya kuwapo sheria hiyo wananchi wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali ikiwamo kukosa fedha zao kutokana na kutokuwapo na sheria inayomlinda mteja.

Alisema hivi karibuni imeshuhudiwa baadhi ya wananchi kupoteza pesa kwenye kampuni ya Master Life pamoja na kutokuwapo kwenye utaratibu wa kifedha.

Mwenyekiti Khadija alisema mara nyingi tasisi ya fedha inapojitokeza athari wanaoathirika zaidi ni wateja hasa wale wenye kipato cha chini waliowekeza fedha zao.

Hata hivyo, alisema kuwa Zanzibar sasa itakuwa na sheria rasmi ambayo itasimamia masuala yote ya huduma ndogo za kifedha ili kuona kila mwananchi aliwekeza anapata haki yake.

"Sasa kutakuwa na sheria makini na itaweka utaratibu wa kusimamia kuona inapojitokeza changamoto pesa za wateja zinapatikana," alisema.

Kwa upande wa SACCOS na Vikoba, alisema sheria hiyo itawezesha na kusaidia kukua kimtaji na kuwasaidia wananchi kwa lengo walilokusudia.

Naye mwanasheria kutoka tume hiyo, Nassor Ameir Tajo, alisema tume hiyo ni chombo cha kiutafiti kwa sheria mbalimbali ili kuhakikisha sheria zote hazileti mgongano kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Alisema kuwa lengo la sheria hiyo ni kuondosha changamoto na malalamiko ya wananchi kuchukuliwa pesa zao na kukimbia kwa baadhi ya tasisi kutoka Tanzania bara kuja Zanzibar na kufanya biashara kwa kuchukua fedha za watu.

Alisema imebainika kuwa hayo yote yanajitokeza kutokana na kuwa na mwanya wa kutokuwapo kwa sheria hiyo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijumuika na waumini wa dini ya Kiislam katika ibada ya sala ya Tarawekh, kwenye Masjid Sunna Rahaleo, jijini Zanzibar juzi. Kushoto ni Katibu wa Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume na kulia kwake ni Kiongozi wa Masjid hiyo, Sheikh Ahmed Haidar Jabir. **PICHA: IKULU**

# ZRB kuendeleza elimu kwa wa'biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BODI ya Mapato Zanzibar (ZRB), imesema itaendelea kuwafikia wafanyabiashara katika maeneo yao ya biashara ili kuwapa elimu ya kodi itakayowahamasisha kulipa kodi kwa hiyari.

Hayo yalielezwa na Ofisa Uhusiano wa Bodi hiyo, Badria Attai Masoud, katika ziara ya utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara wa maduka ya Mombasa ikiwa ni hatua ya bodi hiyo kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi.

Alisema wapo wafanyabiashara wengi wanaokiuka sheria za kodi, hali ambayo inayosababisha mapato mengi ya serikali kupotea.

Aliwataka wafanyabiashara kujua wajibu wao baada ya kusajiliwa kuwa walipa kodi rasmi na kuhakikisha wanatoa risiti kila wanapofanya mauzo yao,kujaza fomu na kufanya malipo kwa wakati.

Ofisa huyo aliwashauri wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na bodi, kujisajili mara moja ili kutambulika kuwa walipakodi halali.

Alisema kufanyabiashara bila kusajiliwa ni makosa makubwa kisheria na serikali haipo tayari kuwafumbia macho wafanyabiashara wote ambao wanakwepa wajibu wao kulipa kodi ambayo inategemewa kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Aidha, alisema lengo la ZRB kutoa elimu ni kufanikiwa katika ukusanyaji wa mapato ya serikali na kujenga mahusiano mazuri kati yao na wafanyabiashara.

"Tulikuwa na utaratibu wa kuwaita wafanyabiashara ofisini kwetu ili kuwapa elimu, lakini mahudhurio yao sio mazuri, ndio tumeona kuwarahisishia huduma kwa kuwafuata katika maeneo yao ya kazi kujenga uhusiano mzuri na kuongeza ari ya ulipaji kodi wa hiyari," alibainisha.

Naye Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Bodi hiyo, Makame Khamis Mohammed, alisema katika zoezi hilo wamekutana na makosa mbalimbali ikiwamo wafanyabiashara kutokuwa na usajili, uwekaji wa kumbukumbu na nyaraka za usajili ikiwamo cheti na kutoa risiti katika utaratibu usioridhisha.

"Wafanyabiashara wengi leo tumewaona hawajui umuhimu wa kutunza kumbukumbu na hata utoaji wa risiti, tumebaini wapo ambao wameanza kutumia kitabu cha risiti tokea mwaka 2019 na sasa ndio wanaendelea kukitumia, lakini tunawaelekeza na kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kuwapa wateja wao risiti," alisema.

Kwa upande wao, wafanyabiashara hao waliipongeza ZRB kuendelea kuwapatia elimu ya kodi ambayo inawasaidia katika harakati zao za biashara za kila siku.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Ali Ali Kombo, aliwaomba wafanyabiashara wenzake kuhakikisha wanalipa kodi na kuiomba ZRB kuwawezesha kimitaji ili kukuza biashara zao na kulipa kodi za serikali kwa urahisi zaidi.

Hivyo waliahidi kuwa watakuwa walimu wazuri kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa ili lengo la serikali la kuleta maendeleo liweze kufikiwa kwa wananchi wote.

# Rais Mwinyi afanya uteuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi katika Vikosi Maalum vya Serikali, Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Katika uteuzi huo, Rais Dk. Mwinyi amemteua Kanali Azana Hassan Msingiri kuwa Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Kanali Makame Abdallah Daima kuwa Mkuu wa Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kanali Rashid Mzee Abdallah kuwa Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Ukozi.

Wengine ni Luteni Kanali, Khamis Bakari Khamis kuwa Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo (Magereza), Luteni Kanali, Burhani Zubeir Nassoro kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na ACP Ahmed Hamis Makarani kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Abdallah uteuzi huo umeanza Aprili, 21,2021.

Mnamo Aprili 12, 2021 Rais Dk. Mwinyi alitengua uteuzi wa Makamanda wa vikosi vitatu vya Idara Maalum za SMZ kufuatia kuwapo kwa wafanyakazi hewa hali iliyosababisha upotevu wa fedha nyingi za Serikali.

Aliowatengua walikuwa ni Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar Ali Abdallah Ali, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kanali Ali Mtumweni Hamad na Mkuu wa Kikosi Maalum cha KMKM Comodore Hassan Mussa Mzee.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 19 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BAHADURALI RAJABALI WALIMOHAMED**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**HASNAIN BAHADURALI RAJABALI WALIMOHAMED**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 Mwezi wa May, 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 14 Mwezi wa April, 2021.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WILLIAM SHILEKARA KIMARO,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili **MC 221CNB .** Injini namba **162FM-JKOCK2403** na Chassis namba **LEAPCK-OE4KK0K2403** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taafifa: **BNG/RB/45/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MAULIDI JOHN MAULIDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 292 CEQ Chassis No.MD2A21-BY6KWL91172,Engine No.PFZWKL12728.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/5320/2021**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**SHAURI LA MIRATHI NO 01 YA 2021**
**1. FESTO IBRAHIM SHAYO…MWOMBAJI**
**2. JOHN RICHAD CHOBO……………………….MWOMBAJI**
**3. WALTER LONGINE……………...MWOMBAJI**
**4. AGATHA LONGINE SHAYO……………………....MWOMBAJI**
**DHIDI**
**DANIEL LONGINI SHAYO……………………….MAREHEMU**
**KWA YEYOTE YULE**
**POPOTE ALIPO**
**KUITWA SHAURINI**

Watajwa hapo juu wamefungua maombi ya kuomba kuteuliwa kuwa wasimamizi wa mirathi ya marehemu Daniel Longini Shayo mahakama hii imepanga kusikiliza shauri hilo mnamo tarehe 07/05/2021, saa 2:30 Asubuhi. Hivyo endapo kama kuna pingamizi lolote lile juu ya shauri hilo liwasilishwe mahakamani tarehe tajwa hapo juu kabla waombaji hawajateuliwa na mahakama hii kuwa wasimamizi wa mirathi.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 21/04/2021

……………………………………..
**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**MWANZA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA. 7/2021**
**AMOS MBWANA MWANSE-LA……………………………………MDAI**
**DHIDI YA**
**1.MANYERERE HAMIS REKOHE……………………………WADAIWA**
**2.FARIDA AMOUR KHALFAN**
**KWA :**
**1.MANYERERE HAMIS REKOHE**
**2.FARIDA AMOUR KHALFAN**

**POPOTE ULIPO- TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI WADAIWA**

Mnatarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya au wakili wenumnamo tarehe 27/04/2021 siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi,ambapo Shauri limepangwa kusikilizwa hukumu.
ELEWA KWAMBA, Mkikosa KUFIKA siku hiyo, shauri hili litasomwa hukumu bila nyiyni kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 20 mwezi 04 mwaka 2021

**HAKIMU MKAZI**
**DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE**
**MBEYA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA. 6/2021**
**EDNAGIDION PIUS………………MDAI**
**DHIDI YA**
**1.MANYERERE HAMIS REKOHE…………………………WADAIWA**
**2.FARIDA AMOUR KHALFAN**
**KWA :**
**1.MANYERERE HAMIS REKOHE**
**2.FARIDA AMOUR KHALFAN**

**POPOTE ULIPO- TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI WADAIWA**

Mnatarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya au wakili wenumnamo tarehe 27/04/2021 siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi,ambapo Shauri limepangwa kusikilizwa hukumu.
ELEWA KWAMBA, Mkikosa KUFIKA siku hiyo, shauri hili litasomwa hukumu bila nyiyni kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 20 mwezi 04 mwaka 2021
**HAKIMU MKAZI**
**DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE**
**MBEYA**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**WINNIE IGNAS RUBARATUKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha **CUHAS-BUGANDO (CATHOLIC UNIVERSITY OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES) kozi ya DEGREE OF DOCTOR OF MEDICINE** chenye namba **CUHAS/MD/4001310/T/14** kilichotolewa mwaka 2019,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **DAR/GOG/RB/194086/2021**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Madereva Dangote sasa warejea kazini

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, amesema serikali itasimamia na kuhakikisha haki za Watanzania katika viwanda mbalimbali nchini zinatendeka na kuwataka waajiriwa kulinda hadhi na heshima ya nchi kwa kuwa waadilifu.

Amesema ustawi wa watu katika nchi huru ni jambo la msingi na Watanzania hawawezi kuwa kama manamba katika nchi yao.

Profesa Kitila alitoa kauli hiyo juzi akiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Godfrey Mwambe, wakati wakizungumza na madereva wa kiwanda cha saruji cha Dangote waliokuwa katika mgomo wa siku ya 12 wakidai maslahi yao.

Alisema serikali mbali na kuwa na jukumu la kulinda haki za Watanzania katika maeneo yao ya kazi ikiwamo viwandani, pia ina jukumu la kuhakikisha wawekezaji wanalindwa na kupewa haki zote za msingi ili wawe mabalozi wazuri kila watakapokwenda.

"Ni jukumu letu serikali kuhakikisha amani inakuwapo vya kutosha na kiwanda hiki cha Dangote kinalindwa sambamba na kulinda maslahi ya wafanyakazi, leo katika kikao cha ndani tumekubaliana mambo manane kati ya kumi mliyokuwa mnalalamikia, ninaamini kwa hatua hii mtarejea kazini na wale wasiotaka kufanya kazi, basi wasiwe chanzo cha vurugu hapa, tutashughulika nao," alisema.

Waziri wa Uwekezaji (Mwambe) alisema siku 12 za mgomo wa madereva ulikuwa na athari hasi kwa wawekezaji kwa kuwa licha ya uzalishaji kuendelea kiwandani, hakukuwa na mzigo uliofikishwa kwa wateja.

"Kipindi hiki mlichoanza kugoma ndiyo Dangote walikuwa na matarajio ya kuanza kupunguza hasara kutokana na kuanza kutumia gesi katika uzalishaji, jambo hili limewasikitisha, ninadhani wakati mwingine kabla ya kukimbilia kugoma mngekuwa na vikao vya majadiliano na waajiri wenu," alisema.

Aliongeza kuwa suala la ajira ya madereva halipo katika mamlaka ya Kiwanda cha Dangote moja kwa moja kwa kuwa wao walikabidhi kazi hiyo kwa mawakala.

Mwambe alisema katika kikao cha ndani na uongozi wa Dangote, uongozi wa kiwanda hicho umekubali kusimamia masuala manane kati ya 10 yaliyokuwa yakilalamikiwa na kwamba watashirikiana na mawakala kusimamia masuala hayo.

Masuala nane yaliyokubaliwa katika kikao cha usuluhishi ni Kampuni ya Dangote iwajibike katika ulipaji wa faini za barabarani zinazotokana na ubovu wa magari na kuongezwa malipo ya safari ya kupeleka mizigo bandarini.

Madai mengine yaliyokubaliwa na uongozi wa Dangote ni pamoja na utengenezaji wa magari kwa wakati pale yatakapoharibika madereva wakiwa safarini, madereva wa Wakala wa Nissa kugawanywa kwa mawakala wengine baada ya wakala wao kufutiwa mkataba, kutoa motisha kwa madereva watakaofanya vizuri kazini na kuwahimiza wateja kutowaweka kwa muda mrefu madereva wanaowapelekea mizigo katika maeneo yao pamoja na ulipwaji wa Sh. 10,000 za kufungia turubai pale wanapopakia mizigo kutoka kiwandani.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, akizungumza kwenye mkutano huo, alisema ikiwa madereva hawatajiunga katika vyama vya wafanyakazi, serikali haitatoa nafasi ya kuwasikiliza pale watakapokuwa na matatizo na mwajiri wao.

Hamad Mzee, mwakilishi wa madereva waliokuwa kwenye mgomo huo, alisema wameridhika na hatua iliyofikiwa na kwamba wako tayari kurejea kazini.

"Yaliyopitishwa sisi madereva tumeridhia lakini ni muhimu mawakala wawe wanatoa nafasi ya kutusikiliza kabla ya kufikia katika hali hii," alisema.

## Kimbunga Jobo chakaribia Lindi

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imesema kimbunga Jobo kinazidi kujiimarisha kaskazini mwa kisiwa cha Madagascar na usiku wa kuamkia leo kilitarajiwa kuwa Km 410 kutoka Mkoa wa Lindi.

Kwa majibu wa taarifa iliyotolewa jana na TMA, uwapo wa kimbunga hicho utaathiri mifumo ya hali ya hewa na kusababisha vipindi vya mvua na upepo mkali ukanda wa Pwani.

"Tunatoa angalizo kwa wananchi kuwa makini hususani wa mikoa ya Lindi, Mtwara na maeneo mengine ya Pwani, waendelee kufuatilia taarifa za mamlaka ili kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na kimbunga Jobo," TMA ilibainisha katika taarifa yake ya jana kwa vyombo vya habari.

Mamlaka hiyo ilisema wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi au usafiri wa majini katika maeneo hayo, wanapaswa kuchukua tahadhari kuepuka maafa.

Juzi, TMA ilitoa taarifa ya dalili ya kuwapo kwa kimbunga hicho kilichoonekana kaskazini mwa kisiwa cha Madagascar huku kikiwa na mwelekeo wa kuja kusini mwa Tanzania Mikoa ya Lindi na Mtwara.

# JKT yajitosa ufugaji samaki

**Na Renatha Msungu,**

MLIMBA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi cha 837 Chita JKT, linatarajia kuanza mradi wa ufugaji samaki aina ya sato, likijipanga kuzalisha tani 12 kwa mwezi na vifaranga 200,000.

Kaimu Kamanda wa Kikosi hicho, Meja Evergreen Bartazal, alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya waandishi wa habari waliotembelea katika kikosi hiko kuona mradi huo.

Meja Bartazal alisema mradi huo utasaidia kutatua kero ya uhaba wa vifaranga vya kutosheleza shamba la Chita pamoja na mashamba mengine ya nje ya kikosi hicho.

Alisema mradi huo kama ungetumia mkandarasi, ungegharimu Sh. milioni 440, lakini kwa kutumia wataalamu wa ndani ya jeshi hilo na vijana, unatarajia kugharimu Sh. milioni 250.

"Tunashukuru mradi huu unaendele vizuri, tunatarajia utaleta matokeo chanya kwa jamii kwa sababu unakwenda kutatua tatizo la uhaba wa vifaranga vya samaki," alisema Meja Bartazal.

Mtaalaam wa Samaki, Luteni Joseph Lyakurwa, alisema katika kikosi hicho wana matangi 27 ambayo hutumika katika kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa samaki.

Alisema matanki hayo yana uwezo wa kuzalisha tani 12 za samaki aina ya sato kwa mwezi na vifaranga 200,000 ambavyo vitatumika kumaliza tatizo la uhaba wa mbegu za samaki.

Mtaalamu huyo alisema bwawa ambalo litakuwa kubwa kuliko mengine nchini na hivyo litasaidia kuongeza upatikanaji wa samaki.

"Mfumo huu wa uzalishaji vifaranga vya samaki kupitia mabwawa yanayojengwa, unalenga kukidhi mahitaji kwa sababu idadi ya watu inaongezeka kushinda vyanzo vya asili vilivyopo," alisema Luteni Lyakurwa.

Alisema kwa sasa bwawa walilonalo linazalisha tani nne za samaki kwa mwezi.

Kijana wa kujitolea wa JKT, William Lubinza, alisema amepata elimu kubwa na atakaporudi uraiani, ataitumia kujipatia kipato bila kutegemea ajira rasmi.

Alisema atakwenda kutoa elimu kwa vijana wengine ambao hawajapata bahati ya kushiriki katika mafunzo ya JKT.



## HABARI MICHEZO

# POCHETTINO AKUNWA KIWANGO CHA ICARDI



**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, alifurahishwa na mabao matatu 'hat-trick' yaliyofungwa na Mauro Icardi wakati wa ushindi wa Jumatano wa 5-0 kwenye Kombe la Coupe de France baada ya kuwa nje ya dimba kwa mwezi mmoja kutokana na kuwa majeruhi.

Icardi alianza kwa mara yake ya kwanza kwa PSG na kuifunga Angers na kufuzu nusu fainali ya kombe hilo.

Raia huyo wa Argentina, ambaye alitumia msimu uliopita akicheza kwa mkopo hapo PSG kutoka Inter kabla ya kusaini mkataba wa kudumu, alikabiliwa na wakati mgumu msimu huu.

"Nina furaha Mauro amefunga mabao matatu usiku huu (juzi)," alisema Pochettino. "mara zote yeye yuko vizuri dimbani, ana nafasi nzuri ya kufunga.

"Amerudi kutoka kukabiliwa na majeraha nina furaha kwa kile alichokifanya."

Icardi amekuwa na wakati mgumu wa kupata namba mbele ya Neymar, Kylian Mbappe, Moise Kean na Angel Di Maria wakiwa ndio chaguo la kwanza.

# Levy alimhofia Mourinho Spurs

**LONDON,** England

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspurs, Daniel Levy anaripotiwa kuwa alikuwa na hofu ya wachezaji kadhaa wa kikosi cha kwanza kuondoka klabuni hapo na akalazimika kumtimua, Jose Mourinho.

Jumatatu, Spurs walitangaza kuwa wametemana na aliyekuwa kocha wao, wakiwa kwenye maandalizi ya kuumana na Man City kwenye fainali ya Kombe la EFL.

Mourinho amekuwa kocha wa Spurs kwa miezi 17, akiwaacha nafasi ya saba nyuma ya West Ham United kwa pointi tano.

Kwa mujibu wa Eurosport, Levy anahitaji kuwabakiza wachezaji kama Harry Kane, Dele Alli na Gareth Bale, na anaamini wangelazimika kuondoka ikiwa Mourinho angesalia klabuni hapo.

Kane amekuwa akihusishwa na kuondoka klabuni hapo, akitajwa kuwavutia Manchester United na Manchester City.

Dele pia anawavutia PSG, lakini Levy angetamani kuendelea kumbakiza ila alikuwa amepoteza mvuto chini ya Mourinho.

Bale licha ya mkataba wake wa mkopo kuelekea mwishoni, Levy anatarajia kuwa wanaweza kumbakiza.

Hivyo, kumtimua Mourinho ilikuwa ni namna ya kujihami na uwezekano wa wachezaji kadhaa kuondoka klabuni hapo.





# Modric akubali kusaini mkataba mpya Madrid

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentina Perez, amebainisha kwamba, klabu hiyo imefikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Luka Modric.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 raia wa Croatia, ambaye alijiunga na Madrid akitokea Tottenham mwaka 2012, mkataba wake unamalizika Juni mwaka huu.

Ripoti za Januari zilibainisha kwamba mkataba mpya kati ya Modric na Madrid umefikiwa, lakini hakuna kilichotangazwa baadaye.

Na sasa Perez alithibitisha Jumatano wakati akijadiliana kuhusu European Super League, huku pia akitoa taarifa kuhusu mkataba wa Sergio Ramos ambao nao unaelekea mwishoni.

"(Modric) tayari amesaini au tumeshafikia makubaliano muda mrefu uliopita," alisema Perez akiambia Redio El Laguaro.

"Hali ya Ramos ipo tofauti. Tumezungumza mara nyingi, sitaki kumlaumu yeyote."

Perez alikataa kuzungumza kuhusu majaliwa ya Ramos mwenye umri wa miaka 35, ambaye ndiye nahodha wa klabu hiyo.

"Nampenda yeye kama mwanangu, nimefanya kila kitu kinachowezekana kwa upande wangu," alisema Perez .

"Sitakuambia chochote kuhusu Sergio Ramos. Tunajaribu kumaliza msimu huu. Halafu tutazungumza nini kitatokea kwa kila mmoja."

# Mashabiki Chelsea sasa wataka uongozi ujiuzulu

**LONDON,** England

MASHABIKI wa Chelsea wanaendelea kutumia shinikizo kwa wanachama wa bodi hiyo kujiuzulu hata baada ya klabu hiyo kujitoa kwenye mashindano mapya ya Ulaya (European Super League).

Mashabiki na wadhamini wa Chelsea wametaka uongozi wa klabu hiyo uondoke madarakani kwa sababu ya madhara ya kudumu ambayo wanaamini yametokana na uongozi wa 'Blues' katika kupigania mashindano hayo.

Mashabiki hao waliandamana nje ya Uwanja wa Stamford Bridge kabla ya mchezo wa sare ya bila kufungana na Brighton, Jumanne.

"Huu ni ushindi mkubwa kwa wafuasi ulimwenguni, mapambano yetu ya kupata mustakabali mzuri wa klabu utaendelea," ilisema taarifa ya mashabiki hao.

"Tunaomba ufafanuzi kamili na wa kina ni kwa nini bodi ilichukua uamuzi wa kuachana na mashindano ya Ulaya na kuelezea kwa nini walijiunga na Super League bila kushauriana na mashabiki wao waaminifu.

"Tumevunjika moyo na kwamba msamaha haujajumuishwa katika taarifa hiyo. Urithi wa klabu yetu uliwekwa hatarini kwa kile kinachoonekana kuwa kwa faida ya kifedha tu.





# ALABA MAMBO SAFI REAL

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa Bayern Munich, David Alaba, amefikia makubaliano ya kujiunga na Real Madrid ya Hispania, kwa mujibu wa Sky Sports.

Alaba anamaliza muda wake katika klabu ya Bayern Munich, na sasa yupo tayari kujiunga na miamba hao wa LaLiga, mwishoni mwa msimu huu.

Alaba anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano na miamba hiyo ya Madrid mpaka mwaka 2026, huku Barcelona wakishindwa mbio hizo.

Mkataba huo unatarajiwa kusainiwa na Alaba na Real Madrid katika wiki kadhaa zinazokuja huku mchezaji huyo akitarajiwa kuondoka kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu.

Alaba ameichezea Bayern Munich katika misimu 13 akiwa ameshinda mataji zaidi ya 12 ikiwamo, Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, mara tisa tisa, Kombe la Ujerumani mara sita na Klabu Bingwa ya Dunia mara mbili.

# *Neymar kupunguziwa mshahara atue Barca*

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR bado yupo katika sintofahamu ya hali yake ya mkataba na Paris Saint Germain, na minong'ono inataja kuwa hatarajii kuongeza mkataba mpya, kwa mujibu wa Marca.

Taarifa zinaeleza ikiwa Neymar hatasaini mkataba mpya na PSG, basi anajiandaa kurejea Barcelona, na atakuwa tayari kukubali punguzo la mshahara wake wa sasa.

Tangu msimu uliopita mshambuliaji huyo wa PSG alikuwa akihusishwa na kurejea Barcelona, lakini masuala ya kifedha yakawa magumu kukamilisha uhamisho wake, kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, kwa sababu ya mlipuko wa corona.

Neymar aliripotiwa kuwa kwenye maendeleo mazuri ya mazungumzo ya mkataba wake, lakini akasitisha mazungumzo hayo.

Taarifa zinaeleza kuwa alipewa muda wa kukamilisha suala hilo, akihitajika kusaini kabla ya mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa Marca, Neymar atakuwa tayari kupunguziwa mshahara ili arejee Barcelona ikiwa hatasaini mkataba mpya na PSG wa kuendelea kuwapo zaidi ya msimu wa 2022.

Nyota huyu wa zamani wa Barcelona, mara nyingi amekuwa akizungumzia nia yake ya kuungana tena na Lionel Messi asmbaye pia alikuwa akihusishwa na PSG. Ikiwa Messi atasalia Barcelona, basi huu unaweza kuwa wakati mwafaka.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE KURUDI CITY FAINALI YA EFL

●●● Majeraha hayakuwa makubwa kama tulivyotegemea, jana (juzi) alionekana kuwa...

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne anaweza kurudi dimbani kuichezea Manchester City kwenye mchezo wa fainali wa Kombe la EFL Jumapili dhidi ya Tottenham Hotspur.

De Bruyne aliumia kifundo cha mguu wakati wa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA wakati wakifungwa bao 1-0 na Chelsea wikendi iliyopita na ilionekana kama engekaa nje ya dimba kwa muda mrefu, lakini sasa anaonekana kuendelea vizuri na anaweza kurudi dimbani Jumapili.

Awali Kocha wa Man City, Pep Guardiola, alisema majeruhi hayo si mazuri kwa mchezaji huyo.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji hakuwapo kwenye mchezo wa ligi wa juzi, Jumatano wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Aston Villa na kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.**

Akizungumzia kuhusu maendeleo yake, Guardiola aliwaambia waandishi wa habari kuwa kuna habari njema kuhusu De Bruyne.

"Majeraha hayakuwa makubwa kama tulivyotegemea, jana (juzi) alionekana kuwa vizuri zaidi," alisema.

"Leo (jana) sikuzungumza naye, lakini naamini hadi kesho (leo) anaweza kuwa vizuri zaidi kwenye mazoezi."

Kama wakishinda taji hilo la EFL Jumapili, watakuwa wameshinda mara nne mfululizo, na baada ya hapo akili zao zitaelekea kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain.

"Nafikiri hayupo tayari kwa fainali, pengine atakuwa tayari kwa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Guardiola.

## ZISIKUPITE

### TUCHEL AMSHANGAA ABRAHAM

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, anaelewa ni kwa nini, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, ana " wasiwasi" na "hasira" kuhusu hali yake. Mshambuliaji huyo wa England, hajaiwakilisha klabu hiyo ya London Magharibi tangu Februari 20, mwaka huu na amehusishwa na taarifa za kuelekea West Ham United. ***(Mail)***

### WILLAN KWENDA MAREKANI

KIUNGO wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 32, amedokeza kuwa na ndoto ya kucheza nchini Marekani, lakini baada ya kushinda taji lolote Arsenal. ***(Goal)***

### BARCA SAFI KWA DEPAY

BARCELONA wameanza mazungumzo ya kumsajili mshambulizi wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 27, mwishoni mwa msimu huu, wakati mkataba wake katika klabu Lyon utakapokamilika. ***(Esport3)***

### KIMMICH AMSAPOTI ALABA

KIUNGO wa kati wa Bayern Munich, Joshua Kimmich, ameunga mkono uhamisho wa mchezaji mwenzake, David Alaba kwenda Real Madrid, akisema hatua hiyo ni muhimu kwa mlinzi huyo wa Austria mwenye umri wa miaka 28. ***(Goal)***

### VARANE KUONDOKA MADRID

HATUA ya David Alaba kuhamia Real Madrid huenda ikimlazimu mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane kuondoka, huku Manchester United wakimfuatilia nyota huyo mwenye umri wa miaka miaka 27. ***(Manchester Evening News)***

### DORTMUND KUMSAJILI SILVA

KLABU ya Borussia Dortmund huenda wakamnunua mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt na Ureno, Andre Silva mwenye umri wa miaka 25, ikiwa watampoteza mshambuliaji wao matata wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Bild)***

### MARCELINO ATAJWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imewasiliana na kocha wa Athletic Bilbao, Marcelino mwenye umri wa miaka 55, katika hatua inayoashiria ni mmoja wa wakufunzi ambao huenda wakamrithi Jose Mourinho, ambaye alifutwa kazi Jumatatu. ***(Athletic)***

### ARSENAL, LEICESTER KWA RICCI

LEICESTER City na Arsenal zipo kwenye mbio moja za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Samuele Ricci mwenye umri wa miaka 19, kutoka klabu ya Empoli. ***(Tuttomercato)***

### QPR WAMTAKA WARBURTON

KOCHA mpya wa Queens Park Rangers, Mark Warburton, mwenye umri wa miaka 58, anakaribia kufikia mkataba mpya ulioboreshwa katika klabu hiyo. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# Tuzo za WIMA 2021 sasa kutolewa Jumamosi

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa pili wa utoaji wa Tuzo za Kuwapongeza Wanawake Viongozi barani Afrika zijulikanazo kama WIMA Awards unatarajiwa kufanyika Jumamosi wiki hii, Mtana Hall LAPF Tower, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa CV People of Tanzania, Naike Moshi, alisema wamelazimika kutangaza tarehe mpya ya utoaji wa tuzo hizo kwa mwaka huu kutokana na mabadiliko yaliyofanyika mwezi uliopita baada ya taifa kukumbwa na msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamburi ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

"Utoaji wa Tuzo za WIMA 2021, sasa utafanyika Jumamosi kwenye ukumbi unaojulikana kama Mtana Hall uliopo LAPF Tower, jijini Dar es Salaam," alisema Moshi.

Tuzo za WIMA zilianzishwa rasmi mwaka 2019 kwa dhumuni la kuwatambua na kuwapongeza wanawake wanaofanya vizuri katika nafasi mbalimbali za uongozi barani Afrika.

"Tunajivunia kuwa sehemu ya hadithi ya mafanikio ya wanawake viongozi mbalimbali hususani hapa nyumbani na nje ya Tanzania kupitia tuzo hizi za WIMA. Kwa mwaka huu tumeongeza vipengele vingine saba ikiwamo SDG Female Champion, WIMA Stem, Next Gem WIMA, "He for She" Leadership, WIMA Abilities, WIMA Lifetime na Exemplary Female Leadership during Covid-19 Crisis, alisema.

Alisema tuzo hizo ni za wazi na kila kipengele wamepatikana washiriki baada ya kuchaguliwa na kupigiwa kura na Umma, mchakato ulilofanyika kwa takriban miezi miwili na ambapo washindi watatangazwa rasmi Jumamosi.

"Nina imani kubwa kuwa tuzo za WIMA zitabaki kuwa kubwa zaidi barani Afrika katika kuwahamasisha na kuwatambua wanawake wanaofanya vizuri katika nafasi mbalimbali za uongozi," alisema.

Kwa upande wa mwakilishi kutoka UN Global Compact Network Tanzania, Marsha Yambi, alisema wanayo furaha kuwa sehemu ya tuzo hizo za wanawake viongozi za WIMA.

"Ni wazi kuwa tuzo hizi zimefungua milango mingi kwa wanawake na mashirika mbalimbali kupata nguvukazi inayoleta matokeo chanya kwa uchumi wa nchi. Hivyo sisi UN Global

# GOMES ACHAMBUA KIWANGO SIMBA USHINDI KAGERA SUGAR

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

PAMOJA na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Goms da Rosa amesema kuwa timu yake haikucheza vizuri hasa kipindi cha pili na kupoteza mipira mingi, lakini anachokiangalia kwa sasa ni kushinda mechi zote Kanda ya Ziwa na kurejea Dar es Salaam wakiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo, Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Kagera, Gomes alisema kuwa timu yake ilitawala mechi kipindi cha kwanza na kupata mabao mawili, lakini kipindi cha pili walikuwa wakipoteza mipira mingi na kuwapa nafasi wapinzani kushambulia, jambo lililowaweka kwenye wakati mgumu.

"Cha muhimu tumeshinda mechi hii. Tumeridhika na ushindi na itatufanya tuwe kwenye hali nzuri na ya kujiamini kwenda kucheza dhidi ya Gwambina FC Jumamosi na baada ya hapo tunarudi kusaka pointi zingine Dar es Salaam.

**"Lengo ni kupata pointi tatu kwenye michezo yangu yote ya ugenini kabla sijarejea jijini Dar es Salaam, makosa madogo madogo ambayo nimeyaona, nitayafanyia kazi ili yasijitokeze katika michezo mingine iliyopo mbele yetu, nina washukuru pia mashabiki wetu kwa ushirikiano ambao wanatuonyesha,"alisema.**

Naye Kocha Msaidizi Selemani Matola, alisema kampeni yao ya kutwaa pointi tisa Kanda ya Ziwa inakaribia kukamilika, kwani tayari wameshakusanya sita na sasa zimebaki tatu tu ili wafunge mahesabu.

"Ukweli si rahisi sana, kwa sababu umeona mwenyewe mechi mbili ambazo tumecheza, hazikuwa nyepesi. Tumebakisha dhidi ya Gwambia. Haitokuwa mechi rahisi, lakini tumejipanga kuhakikisha tunapata na hizo tatu zilizobaki," alisema Matola.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, alisema kuwa awali alianza na mfumo wa mabeki watatu nyuma, kitu ambacho kiliwapa nafasi Simba kushambulia sana kipindi cha kwanza na kupata mabao mawili ya haraka haraka, lakini alibadilisha mfumo kipindi cha pili ambapo mambo yalienda vizuri kidogo, lakini si kwa vile walivyohitaji.

"Kipindi cha pili niliongeza kiungo mshambuliaji na kuchezesha mabeki wanne, hali ilitulia, lakini ni lazima tujue kuwa Simba ni timu kubwa na yenye wachezaji wenye uwezo wa hali ya juu, hivyo si rahisi sana kuwazuia wakati wote," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

NIMETUSUA...




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Linus Gasper Shayo, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 21.3 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13. Kwa sasa Jackpot ya SportPesa imefika Sh. 237,953,180. **PICHA: SPORTPESA**

# *Gwambina yaipigia hesabu Simba kesho*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Gwambina FC, Mohammed Badru, amesema ameanza kuifanyia kazi kasi ya uchezaji wa Simba hususan safu ya ushambuliaji, kwa kuwapa mbinu mbadala mabeki wake jinsi ya kukabiliana na wapinzani wao hao ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Badru alisema amewafuatilia vizuri Simba wanavyocheza na anafahamu ni timu bora iliyoimarika kila idara hali inayomfanya kuhakikisha anaiandaa vema safu yake ya ulinzi ili kuwazuia washambulaji wa wapinzani wao hao wakiongozwa na Meddie Kagere.

Alisema Simba iko vizuri hasa kila idara huku washambuliaji wao wakiwa tishio kwa mabeki pinzani, jambo ambalo anafanyia kazi kwa safu yake ya ulinzi kuhakikisha haifanyi makosa na kuruhusu ngome yao kutikiswa.

"Tunakutana na Simba kwa hapa kwetu ni timu bora sana kwa sababu ya uimara wao kila idara. Tumepoteza michezo miwili, KMC FC na Yanga zote ugenini, ila kwa Simba nina imani tutapambana kutafuta matokeo chanya kwa sababu nimewaona jinsi wanavyocheza na uimara wao," alisema Badru.

Michezo
Ijumaa Aprili 23, 2021
Nipashe



De Bruyne kurudi City fainali ya EFL UKURASA 22

AIR MANULA...



Kipa wa Simba, Aishi Manula, akiwa mazoezini na mlinda mlango namba tatu wa timu hiyo, Ally Salim (Jezi namba 30), timu hiyo inajiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Gwambina FC keshokutwa, Jumamosi. **PICHA: MAKTABA**

# Manula atoa siri ukuta kisiki Wawa, Onyango

## ●●● Awataja pia Kapombe, Tshabalala akianika nia yake kwenda kucheza soka nje kuwa...

**Na Mwandishi Wetu**

MLINDA mlango namba moja kwa ubora nchini kwa sasa, Aishi Manula 'Air Manula', ameanika siri ya mafanikio ya kujenga ukuta imara akiwa na mabeki wake namba moja wa kati, Mkenya Joash Onyango na Muivory Coast Pascal Wawa katika klabu ya Simba.

**Hadi sasa katika Ligi Kuu Bara, Manula ndiye kipa anayeongoza kwa kumaliza mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean Sheet' akiwa nazo jumla 13 katika mashindano yote msimu huu.**

Ubora wa Manula umeiwezesha Simba kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiongoza Kundi A, lililokuwa likizijumuisha, mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan, ambapo ameruhusu mabao mawili tu katika mechi sita alizocheza.

Kiwango alichokionyesha katika michuano hiyo, pia kimemfanya kuwa kipa namba mbili aliyeruhusu mabao machache zaidi kwenye makundi yote manne ya Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya kipa wa Wydad Casablanca aliyeruhusu bao moja pekee.

Lakini pia katika Ligi Kuu, ameiwezesha Simba kuwa timu pekee hadi sasa iliyoruhusu mabao machache zaidi (tisa pekee) kati ya timu zote 18 zinazoshiriki ligi hiyo msimu huu wakati huu timu yake ikishika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 55, mbili nyuma ya vinara Yanga iliyopo kileleni, lakini ikiwa mbele michezo mitatu.

Akizungumzia ubora wake msimu huu na safu ya ulinzi ya timu hiyo, Manula amesema yeye si kitu pasipo ushirikiano mkubwa kutoka kwa mabeki wake husan wa kati, Onyango na Wawa wakishirikiana na mabeki wa pembeni, Shomary Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

"Onyango, Wawa, Tshabalala na Kapombe, mara zote huwa nawaambia bila wao mimi si kitu, mara zote huwa tunazungumza kwanza kuwa tunaanza kupambana tusiweze kufungwa, tunaambiana na kukumbushana mara kwa mara.

"Mara nyingine tunatumia lugha ya ukali, lakini tunaelewana, kikubwa ni kushirikiana na kukumbushana, ila kadri tunavyocheza pamoja tunajuana vizuri, hivyo wanapokosea wanategemea mimi kurekebisha," alisema.

Manula alisema kadri wanavyozidi kucheza pamoja kumesaidia kuzidi kuelewana na kujuana na kwamba inakuwa rahisi kuweza kutimiza majukumu yao uwanjani.

"Kucheza pamoja kumetusaidia kujuana vizuri, hata mpira uliopigwa unaweza kujua huu utampita Wawa ama Onyango ama ule mpira Manula haufikii, hivyo tunajipanga.

Kuhusu matarajio yake na ya klabu, Manula alisema ni makubwa na la kwanza ni kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa ligi na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na ikiwezekana kuvuka lengo hilo, na lengo la tatu likiwa ni yeye binafsi kuweza kutoka nje ya Simba ama Tanzania.

"Kuhusu Al-Merrikh sijui lolote kwa sababu mimi bado ni mchezaji wa Simba, na klabu kubwa zinajua zinapotaka mchezaji zinafanyaje, kwani zinapaswa kwenda kwanza kwa klabu ndipo klabu imfuate mchezaji husika," alisema Manula.

# Rais aahidi kupaisha michezo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu, amesema serikali anayoiongoza itaanza kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kuziandaa timu za Taifa.

Akihutubia bunge jana, Rais Samia alisema timu hizo ni pamoja na za wanawake.

"Tumechoka kuitwa jina lile alilosema Mzee Mwinyi ['kichwa cha mwendawazimu'] kuwa tunaenda nje na ushabiki mkubwa tukirudi vichwa chini, tutajitahidi kuangalia sekta hiyo ipate msukumo na kupandisha hali za wachezaji ili Tanzania tuingie kwenye ramani za football ['soka'],"alisema.

Alisema sekta ya michezo, sanaa na utamaduni inakua kasi kubwa na wengi wamepata ajira kupitia sekta hiyo, hivyo kama ilivyoahidiwa kwenye ilani ya uchaguzi serikali itatekeleza.

"Kwenye miaka hii mitano tunalenga kukuza sekta ya sanaa na michezo kwa kuimarisha hati miliki ili wasanii wanufaike na kazi zao, kuhuwisha mfuko wa utamaduni na sanaa ili wasanii wetu wapate mafunzo na mikopo, tutaanza kutenga fedha kwa timu zetu za taifa,"alisema.

Samia pia alisema ataendelea kuwapa nafasi wanawake katika uongozi, lakini akasisitiza vigezo vinavyojumuisha uwezo na elimu vitazingatiwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >